**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2008/09 ILIYOTOLEWA KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI NA WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA MAZINGIRA MHE. BURHAN SAADAT HAJI (MBM)

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2008/09 ILIYOTOLEWA KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI NA WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA MAZINGIRA MHE. BURHAN SAADAT HAJI (MBM)

## 1.0 UTANGULIZI

1.1 **Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwa Baraza lako Tukufu, likae kama Kamati ili kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2008/09.

1.2 **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutukutanisha tena tukiwa na afya njema na uzima na kuijaalia nchi yetu amani na utulivu. Kwa niaba ya wafanyakazi wenzangu wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira napenda kumpongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dk. Amani Abeid Karume kwa uongozi wake mzuri, wa hekima na busara. Aidha, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa heshima kubwa aliyopewa na Chuo Kikuu cha Taifa cha South Carolina, Columbia Marekani kwa kupewa shahada ya Udaktari wa Falsafa katika Fani ya Sheria. Hii inatokana na mchango wake mkubwa katika kuimarisha utawala bora na demokrasia pamoja na kupunguza umaskini Zanzibar.

1.3 **Mheshimiwa Spika,** shukurani za pekee ziende kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika. Hii inatokana na uongozi wake mzuri na uhodari wake wa kusimamia amani na kuleta usuluhishi sehemu mbali mbali barani Afrika.

1.4 **Mheshimiwa Spika,** naomba kumpongeza Waziri Kiongozi, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kuwa mshauri na mfuatiliaji wa maendeleo ya kilimo Zanzibar. Aidha nampongeza kwa kazi zake nzuri anazozifanya katika Sekta ya Kilimo hasa kwa kufanya ziara na kutoa maelekezo mazuri yanayosaidia kuendeleza sekta hii.

1.5 **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii kutoa pongezi kwa Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Ali Juma Shamuhuna kwa juhudi na ushauri wake mzuri wa kuendeleza sekta ya kilimo. Michango yake katika kuimarisha Sekta ya Kilimo Zanzibar ni ya kupigiwa mfano.

1.6 **Mheshimiwa Spika,** napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kazi zako za kuliendesha Baraza lako Tukufu. Aidha, nawashukuru wajumbe wa Baraza lako Tukufu pamoja na kamati zake zikiwemo Kamati ya Fedha na Uchumi, Kamati ya Kufuatilia Ahadi za Serikali na Kamati ya Ukaguzi na Udhibiti wa Hesabu za Serikali kwa michango, ushauri, mashirikiano na ufuatiliaji wao kwa kipindi cha mwaka 2007/08.

1.7 **Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa pongezi za dhati kwa viongozi na wanachama wa CCM wa Jimbo la Kikwajuni kwa kushirikiana na kufanikisha vizuri maendeleo ya jimbo.

## 2.0 UPUNGUFU WA CHAKULA DUNIANI

2.1 **Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua fursa hii kutoa taarifa ya upungufu wa chakula duniani na vipi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejiandaa kukabiliana na hali hii.

2.2 **Mheshimiwa Spika**, hivi sasa dunia inashuhudia upungufu wa chakula na upandaji wa bei za vyakula kama vile mchele na ngano. Hii imesababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa, kushuka kwa uzalishaji, kupanda kwa bei ya mafuta, kupanda kwa gharama za uzalishaji, kuzalisha mazao ya kilimo kwa ajili ya nishati ya kibaolojia, kuongezeka kwa idadi ya watu na kushuka kwa upatikanaji wa mbolea. Hali hii imesababisha matatizo makubwa ya upungufu wa chakula duniani hasa kwa nchi zinazoendelea ikiwemo Zanzibar.

2.3 **Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na hali hii, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar ameunda Kamati Maalum yenye lengo la kuhakikisha Zanzibar inaimarisha kilimo na kuwa na chakula cha kutosha na cha bei nafuu. Aidha, amefanya ziara katika maeneo ya Sekta ya Kilimo na kujionea hali ya uzalishaji.

2.4 **Mheshimiwa Spika,** napenda kulijuulisha Baraza lako Tukufu kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mwaka huu wa fedha 2008/09 itatoa ruzuku kwa asilimia 50 ya bei ya mbolea ili kuwasaidia wakulima kuwa na uwezo wa kununua mbolea kwa bei nafuu na kuongeza uzalishaji hasa katika kipindi hiki cha upungufu wa chakula duniani. Aidha, Wizara kwa kupitia miradi na programu za Uhakika wa Chakula na Lishe, PADEP, ASSP, ASDP-L, MACEMP, Miradi ya Umwagiliaji maji na TASAF inaendelea kuwasaidia wananchi kuongeza ufanisi katika uzalishaji.

2.5 **Mheshimiwa Spika,** natoa wito kwa wananchi wote Unguja na Pemba wakiwemo Waheshimiwa Wawakilishi wa Baraza lako Tukufu kuendeleza

juhudi za kilimo ili kila mmoja wetu atoe mchango wake katika kuongeza uzalishaji katika sekta hii – "TULIME KWA BIDII"

**3.0 ATHARI ZA UMEME KATIKA SEKTA YA KILIMO**

**3.1** **Mheshimiwa Spika,** kama tunavyofahamu ukosefu wa umeme uliathiri maeneo mengi yakiwemo ya sekta ya kilimo. Umeme katika sekta ya kilimo unatumika kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji maji (pumps); mifugo (Uhifadhi wa maziwa, nyama na uzalishaji wa vifaranga) na uvuvi (kuhifadhi mazao ya baharini na mawasiliano katika doria za baharini).

**3.2** **Mheshimiwa Spika,** naommba kuliarifu baraza lako tukufu kwamba Wizara ilishirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kukabiliana na Majanga (UNDAC) na kufanya tathmini ya athari ya ukosefu wa umeme katika sekta ya kilimo.

**3.3** **Mheshimiwa Spika,** tathmini hiyo imeonesha kwamba mabonde ya umwagiliaji maji ya Bumbwisudi na Kibokwa yaliathirika kwa kukosa huduma za maji kutokana na ukosefu wa umeme. Jumla ya hekta 180 zenye uwezo wa kuzalisha wastani wa tani 1,033 za mpunga zimeathirika. Maji yakipatikana mazao haya yanaweza kuokolewa.

**3.4** **Mheshimiwa Spika,** kutokana na hali hii Mheshimiwa Rais wa Zanzibar Dk. Amani A. Karume alitembelea maeneo hayo na kuwapatia majenereta na transfoma katika mabonde hayo ili kuwapa nguvu wakulima ya kuendeleza kilimo cha mpunga na mbogamboga. Naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa jitihada zake za kuokoa hekta 128 (sawa na asilimia 71 ya hekta zilizoathirika) zisiharibike na kutawawezesha wakulima kuzalisha mpunga wenye wastani wa tani 734.

**3.5** **Mheshimiwa Spika,** bonde la Cheju lenye hekta 52 lenye uwezo wa kuzalisha mpunga wastani wa tani 298 limeathirika zaidi kwani hata kama maji yatapatikana mazao hayo yameshapotea. Kutokana na hali hiyo Wizara imewasiliana na Shirika la Chakula Duniani (FAO), Shirika la Mpango wa Chakula (WFP), Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD) na Shirika la Misaada la Marekani (USAID) ili kuweza kupata misaada ya mbolea, mbegu, majenereta, chakula na fedha ili kuweza kuwasaidia wakulima wa Cheju kurejesha uzalishaji kwa msimu ujao.

**4.0 HALI YA UZALISHAJI WA MAZAO YA CHAKULA**

**4.1** **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai 2007 hadi April 2008 takwimu za hali ya hewa zinaonyesha kwamba mvua zilizonyesha ni kidogo (milimita 2,409.3)

ikilinganishwa na mvua za mwaka uliopita ambazo zilikuwa milimita 2,742.6. Aidha takwimu hizo zinaonyesha kuwa kisiwa cha Unguja kilipata mvua nyingi zaidi (milimita 1,744.2) ukilinganisha na kisiwa cha Pemba (milimita 665.1) (**Kiambatisho 1).**

4.2 **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2007/08 Sekta ya Kilimo imechangia kwa asilimia 27.3 katika Pato la Taifa (GDP) ambapo mazao ya kilimo yamechangia asilimia 16.9, uvuvi 5.6, mifugo 4.4 na misitu 0.4. Licha ya kuonekana Sekta ya Kilimo iko nafasi ya pili katika kuchangia Pato la Taifa ikitanguliwa na Sekta ya Huduma asilimia 43.9 (biashara 9.5, utalii 7.8, usafiri 6.9, na huduma nyengine) bado Sekta ya Kilimo inabakia kuwa uti wa mgongo wa Taifa letu.

4.3 **Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla, takwimu zinaonesha hali ya uzalishaji kwa mazao muhimu ya kilimo kwa mwaka 2007 imeshuka kwa asilimia 5.3 ukilinganisha na mwaka 2006 **(Kiambatisho 2)**. Hii inatokana na sababu zifuatazo:-

- Kupanda kwa gharama za mbolea
- Upungufu wa mbegu bora.
- Mabadiliko ya hali ya hewa yasiotabirika
- Mashambulizi ya maradhi ya ukungu wa muhogo "cassava brown streak" katika muhogo.
- Eneo la kilimo lililolimwa kwa baadhi ya mazao lilikuwa dogo.
- Uhaba wa matrekta

4.4 **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa kilimo cha umwagiliaji maji eneo la hekta 640 sawa na asilimia 8 ya hekta 8,521 zilizoainishwa katika Mpango Mkuu wa Umwagiliaji Maji ndizo zinazolimwa kwa mazao ya mpunga na mboga mboga. Kiasi cha tani 3,673.6 za mpunga sawa na mchele tani 2,204 zinazalishwa katika maeneo hayo. Kilimo cha umwagiliaji maji kina uwezo wa kuzalisha wastani wa tani 5.74 kwa hekta, lengo ni kufikia tani 6.5 kwa hekta iwapo miundo mbinu ya umwagiliaji maji itaimarishwa, mbolea, mbegu na huduma zinazotolewa shambani zitafuata kiwango cha kitaalamu kinachotakiwa. Kwa sasa jumla ya kaya 3,088 Unguja na Pemba zinafaidika na Mpango huu na hivyo kunufaisha watu 15,440.

4.5 **Mheshimiwa Spika**, Hii inaonesha ikiwa maeneo yote 57 yenye hekta 8,521 yaliyoainishwa katika Mpango Mkuu wa Umwagiliaji Maji Zanzibar yatalimwa kikamilifu yanaweza kuzalisha tani 73,365 za mpunga ambapo ni sawa na mchele tani 44,019 kwa mwaka na kutasaidia kwa kiasi kikubwa kuwa na

Uhakika wa Chakula na kutoa ajira kwa kaya 41,114 na kuwanufaisha watu 205,569.

4.6 **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa uvuvi na mazao ya baharini, jumla ya tani 23,581.6 za samaki zenye thamani ya TShs. 34,639,223,250 zimevuliwa kwa mwaka 2007 ambazo ni ongezeko la asilimia 2.4 ikilinganishwa na tani 23,105 zilizovuliwa mwaka 2006 zenye thamani ya TShs. 29,836,611,031. Aidha, jumla tani 8,485 za mwani (cottonii tani 63.8 na spinosum tani 8,421.2) zimezalishwa kwa mwaka 2007 na kuwawezesha wananchi kujipatia jumla ya Tsh 1,321,251,500. Uzalishaji huo umeongezeka kwa asilimia 10.5 ukilinganishwa na uzalishaji wa tani 7676 mwaka 2006 zenye thamani ya Tshs. 925,201,809. Hii imechangia kwa kiasi kikubwa kuongeza kipato na kupunguza umasikini kwa wananchi wengi hasa wa ukanda wa pwani na wanaojishughulisha na uvuvi na ukulima wa mwani.

4.7 **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa sekta ya mifugo, jumla ya ng'ombe 14,828 wamechinjwa ambapo 5,104 kutoka hapa Zanzibar na 9,724 wameingizwa kutoka Tanzania Bara na kufanya jumla ya tani 70.18 za nyama ya ng'ombe. Aidha jumla ya mbuzi 996 wamechinjwa na kuzalisha tani 5.2 za nyama ya mbuzi. Kwa upande wa kuku, jumla ya kuku 384,058 wamechinjwa na kuzalisha nyama ya kuku tani 230.4. Aidha, jumla ya lita 1,642,500 za maziwa, ngozi 5,300 na mayai 3,285,000 zimezalishwa.

## 5.0 MKAKATI WA KUKUZA UCHUMI NA KUPUNGUZA UMASIKINI

5.1 **Mheshimiwa Spika,** katika suala zima la kukuza uchumi na kupunguza umasikini, Sekta ya Kilimo ina mchango mkubwa katika kunyanyua uchumi na kupunguza umasikini hasa kwa wananchi wa vijijini. Programu na miradi ya Sekta ya Kilimo imewawezesha wakulima, wafugaji na wavuvi kwa kuwapa huduma, nyenzo na taaluma ili kuongeza uzalishaji na kipato.

5.2 **Mheshimiwa Spika,** fedha zilizotumika kuwasaidia wakulima moja kwa moja kupitia miradi ya Sekta ya Kilimo ni kama ifuatavyo:

- **MACEMP- Tshs. 1,617,590,434.**
- **PADEP- Tshs. 1,175,235,293.**
- **ASSP – Tshs. 136,985,000.**
- **ASDP-L – Tshs. 58,340,000.**

## 6.0 UTEKELEZAJI 2007/08 NA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA 2008/09

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira imetekeleza malengo ya mwaka 2007/08 kupitia taasisi zake, ambazo ni Idara saba, Kamisheni na Karakana ya Matrekta kama ifuatavyo:-

## 6.1 IDARA YA SERA NA MIPANGO

**Mheshimiwa Spika,** Idara hii ina majukumu ya kusimamia na kuratibu taasisi za ndani na nje ya Wizara, mashirikiano na taasisi za Serikali ya Muungano, Jumuiya za Kikanda na Washirika wa Maendeleo katika Sekta ya Kilimo. Idara inasimamia ukusanyaji wa mapato na matumizi, utumishi na mafunzo kwa wafanyakazi, utayarishaji na usimamizi wa sera, sheria, mikakati na programu za maendeleo katika Sekta ya kilimo.

### 6.1.1 UTEKELEZAJI WA MALENGO 2007/08

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2007/08 Idara imetekeleza yafuatayo:-

- Hadi kufikia mwezi wa Aprili, 2008 jumla ya TShs. 399,843,684 zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 57 ya lengo.
- Kitengo cha tahadhari za mapema kimeimarishwa kwa kupatiwa vitendea kazi vikiwemo komputa mbili, pikipiki na digital camera.
- Kitengo cha uwekaji wa kumbukumbu kimeanzishwa ambapo wafanyakazi watatu wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi.
- Wizara imeanzisha **tovuti (Website)** ambayo anuani yake ni www.kilimo.zanlink.org. Tovuti hii itasaidia kutangaza mambo duniani yanayohusu maendeleo na mikakati ya Sekta ya Kilimo Zanzibar. Aidha, itatoa taarifa zinazohusu sera, masoko, bei za bidhaa, taarifa za tahadhari za majanga. Pia itakuwa ni kiungo cha taarifa za mambo mbali mbali ya Serikali kama vile MKUZA, miradi na programu nyengine.
- Jengo la Makao Makuu ya Wizara limekarabatiwa, sambamba na ununuzi wa samani na vifaa vyengine vya kufanyia kazi.
- Wafanyakazi 175 wamepatiwa nafasi za masomo ndani na nje ya nchi (wanaume 129, wanawake 46) hadi sasa wanaoendelea na masomo nje ni 87 (wanaume 70, wanawake 17) na ndani 88 (wanaume 60, wanawake 28).
- Wafanyakazi wanaoendelea na masomo ya muda mrefu 80 (wanaume 59, wanawake 21). Viwango vya elimu vinavyochukuliwa kwa sasa ni pamoja na PhD 1, shahada ya pili 10(wanaume 6, wanawake 4), shahada ya kwanza 12 (wanaume 7, wanawake 5), stashahada 27 (wanaume 22, wanawake 5) na cheti 30 (wanaume 13, wanawake 17). Aidha masomo ya muda mfupi yametolewa kwa wafanyakazi 93 (wanaume 70, wanawake 23)
- Hatua za marekebisho ya mishahara kwa watumishi wote wa Serikali zimefanywa ili kuongeza maslahi ya watumishi wa Wizara.

- Sera na Programu ya Uhakika wa Chakula na Lishe imeshakamilika na taratibu za matayarisho ya sheria yameanza. Wizara inatoa shukurani kwa michango mizuri iliyotolewa na Waheshimiwa Wawakilishi wakati wa kupitisha sera hii.
- Kitengo cha Uhakika wa Chakula na Lishe kitaanzishwa baada ya kukamilika kwa sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe
- Idara inaendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa programu za Kuimarisha Huduma za Kilimo na Mifugo- ASSP na ASDP-L
- Sera ya Sekta ya Kilimo imetangazwa kwa washirika mbali mbali na Idara inaendelea na juhudi ya kuchapisha na kuisambaza kwa washirika
- Idara imetayarisha miradi mipya 12 ya maendeleo ya sekta ya kilimo na tayari imewasilishwa kwa Washirika wa Maendeleo.
- Wizara inaendelea kushirikiana na washirika wa maendeleo wakiwemo FAO, ADB, WB, IFAD, JICA, KOICA, WFP, WSPA, IAEA, UNDP, USAID, CARE, GF, EU. Aidha, mashirikiano ya kikanda yameendelezwa kwa EAC, SADC na AU. Pia mashirikiano yameendelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Japan, Korea, China, Iran, Egypt, Oman, Norway na Finland

### 6.1.2 MALENGO 2008/09

**Mheshimiwa Spika,** Idara inatarajia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya TShs. 696, 702,000 kutoka vyanzo mbali mbali vya mapato.
- Kutengeneza rasimu ya sheria itayopelekea kuundwa na kufanyakazi kwa Divisheni ya Uhakika wa Chakula na Lishe
- Kuhamasisha uelewa wa Sera na Programu ya Uhakika wa Chakula na Lishe katika ngazi za Taifa, Wilaya na Jamii
- Kujenga uwezo wa Wilaya na Jamii kupanga mipango ya maendeleo inayozingatia suala la Uhakika wa Chakula na Lishe.
- Kukusanya takwimu za mazao ya chakula na biashara
- Kufanya tathmini ya upatikanaji wa Chakula kwa Unguja na Pemba
- Kutengeneza Sera na Mkakati wa Masoko ya Kilimo
- Kuwaombea ajira ya kudumu wafanyakazi 451 wa kutwa na kusimamia maslahi ya wafanyakazi.
- Kufanya mapitio na kusimamia Sera na Sheria zilizo chini ya Sekta ya Kilimo.
- Kutayarisha Mpango Mkuu wa Utafiti wa Wizara (Research Master Plan)
- Kuendelea kusimamia programu za ASSP na ASDP-L
- Kusimamia miradi mipya ya Usarifu wa Mazao (Agro-processing), Mradi wa Miundo Mbinu ya Sekta ya Kilimo.
- Kusimamia Programu ya Uhakika wa Chakula na Lishe.
- Kutayarisha mahitaji ya masomo ya wafanyakazi wa Wizara na kuendelea kuwapatia nafasi za masomo ndani na nje ya nchi.
- Kuendeleza mashirikiano na taasisi za kitaifa na kimataifa zinahusika na Tahadhari ya Mapema.

### 6.1.3 MIRADI NA PROGRAMU

**Mheshimiwa Spika,** Idara imesimamia programu nne kama zifuatazo:

- Programu ya Kuimarisha Huduma za Kilimo –ASSP **(Kiambatisho 3)**
- Programu ya Kuimarisha Huduma za Mifugo -ASDP-L **(Kiambatisho 4)**
- Programu ya Uhakika wa Chakula na Lishe – FSNP **(Kiambatisho 5)**
- Programu ndogo ya kuhamasisha na kutoa mafunzo ya UKIMWI

#### 6.1.3.1 Programu ndogo ya Kuhamasisha na Kutoa Mafunzo ya UKIMWI

**Mheshimiwa Spika,** kama zilivyo taasisi nyengine za Serikali na za Kijamii, Wizara yangu pia haiko nyuma katika harakati za mapambano dhidi ya janga la UKIMWI. Wizara inaendelea na kutoa elimu ya UKIMWI kwa wafanyakazi wake pamoja na wazalishaji wote katika Sekta ya Kilimo, ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, wavuvi, wanamazingira na wanaushirika.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu kwa kushirikiana na Tume ya Ukimwi ya Taifa ilipanga kufanya utafiti wa kuainisha makundi yalio katika hatari ya kuambukiza VVU miongoni mwa washirika wetu wakuu na mambo yanayochangia maambukizo hayo, athari za Ukimwi na kuainisha fursa ziliomo ndani ya Wizara yangu zitakazosaidia kupambana na UKIMWI. Wizara pia ilitoa mafunzo kwa makundi yaliyo katika hatari ya kuambukizwa kama vile wavuvi katika sehemu za dago, kambi za ukulima na za uchumaji wa karafuu.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara imewafundisha waelimishaji rika 65 katika idara zake za Unguja na Pemba wanaosaidia harakati hizi. Aidha jumla ya wafanyakazi 600 wa Wizara tayari wameshapatiwa mafunzo ya Ukimwi Unguja 280 (wanaume 128 na wanawake 152) na Pemba 320 (wanaume 212 na wanawake 108)

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2008/09 Idara ya Sera na Mipango inatarajia kuratibu na kusimamia miradi mipya miwili:

#### 6.1.3.2 Mradi wa Miundombinu ya Sekta ya Kilimo

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu una lengo la kujenga miundombinu ya Sekta ya Kilimo Unguja na Pemba. Miundombinu inayopewa kipa umbele ni pamoja na ujenzi wa masoko, miundombinu ya umwagiliaji, machinjio, barabara za mashambani (feeder roads), maabara za utafiti wa kilimo na majengo ya taasisi za Sekta ya Kilimo. Mradi huu unasaidiwa na ADB na SMZ.

6.1.3.3 **Mradi wa Usarifu wa Mazao (AGRO PROCESSING)**

**Mheshimiwa Spika**, mradi una lengo la kujenga kituo cha mafunzo katika Chuo cha Kilimo Kizimbani kitakachokuwa na mashine za kusarifu mazao pamoja na maabara ya kisasa itakayohakikisha ubora na udhibiti wa viwango kwa mazao yanayosarifiwa.

**Mheshimiwa Spika,** kituo kitatoa mafunzo ya usarifu wa mazao ya kilimo na huduma za udhibiti na ubora wa viwango kwa wanafunzi wa Chuo cha Kilimo Kizimbani, pamoja na wazalishaji wadogo wadogo na wakati (SMEs). Pia kitasajili wajasiriamali watakaopatiwa huduma hizi ikiwa ni katika jitihada za kukuza ajira na kupunguza umasikini. Mradi huu unasaidiwa na KOICA na SMZ.

**6.1.4 MTAZAMO WA BAADAE**

**Mheshimiwa Spika,** Idara inatarajia kuongeza ufanisi katika majukumu yake kwa kuanzishwa kwa Divisheni ya Uhakika wa Chakula na Lishe itakayosimamia na kuratibu uzalishaji, uagizaji na matumizi ya chakula. Aidha, divisheni hii itakwenda sambamba na MKUZA kwa kushirikiana na washirika wake wote. Idara pia ina mpango wa kuimarisha masomo ya ngazi ya juu, itaongeza idadi ya wataalamu katika Sekta ya Kilimo ili kunyanyua uzalishaji wa mazao ya kilimo ambapo itaongeza pato la wananchi na Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Idara pia ina nia ya kutekeleza Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania (Joint Assistance Strategy for Tanzania – JAST) kwa kusimamia miradi na program za Wizara.

**6.2 KAMISHENI YA KILIMO, UTAFITI NA ELIMU KWA WAKULIMA**

**Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ina jukumu la kusimamia na kuratibu kazi zote za Kilimo, Utafiti na Elimu kwa Wakulima zikiwemo kazi za upatikanaji na usambazaji wa pembejeo na zana za kilimo, ukaguzi na uhifadhi wa mazao, kazi zote za utafiti na utoaji mafunzo kwa wakulima. Katika kutekeleza majukumu hayo Kamisheni inasimamia na kuratibu kazi za kawaida na za maendeleo ya sekta zake kama ifuatavyo:-

**6.2.1 KILIMO**

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Kilimo kupitia kitengo cha Mpunga na Pembejeo kina jukumu la kuzalisha mbegu za mpunga, mahindi, jamii ya kunde na mboga mboga. Pia kununua na kusambaza mbolea na kutoa huduma za matrekta kupitia jumuiya za wakulima. Kazi nyengine ni kuwahamasisha wafanyabiashara ili waweze kutoa huduma na pembejeo kwa wakulima.

#### 6.2.1.1 UTEKELEZAJI WA MALENGO 2007/08

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2007/08 kitengo kimetekeleza yafuatayo:-

- Ekari 18,870 za mpunga zililimwa Unguja na Pemba sawa na asilimia 75 ya lengo ambapo ekari 6,991 zimelimwa kwa trekta, ekari 11,850.75 zimelimwa kwa mkono na ekari 28.25 zimelimwa kwa jembe la kukokotwa na ngo'mbe.
- Tani 13 za mbegu ya mpunga zimezalishwa na kusambazwa kwa wakulima sawa na asilimia 130 ya lengo
- Kitengo kilizalisha tani 7.5 za mbegu ya mahindi na mboga mboga hii ni sawa na asilimia 93.7 ya lengo
- Tani 130 za mbolea zilinunuliwa na kuuzwa kwa wakulima wa Unguja na Pemba.
- Matrekta 13 yalitengenezwa na kununua majembe ya kuchimba 5.
- Mabwana shamba 18 na wakulima 30 kutoka wilaya zote za Unguja na Pemba wamepatiwa mafunzo ya kilimo cha maksai.
- Matrekta 12 na power tiller 12 mapya na zana zake pamoja na vifaa vya umwagiliaji maji vimenunuliwa na yanatarajiwa kufanyakazi katika msimu ujao.

#### 6.2.1.2 MALENGO 2008/09

**Mheshimiwa Spika,** Kitengo cha Mpunga na Pembejeo kinalenga kutekeleza yafuatayo:

- Kusimamia ukulima wa mpunga ekari 25,000,
- Kuzalisha na kusambaza tani 10 za mbegu ya mpunga, tani 8 za mbegu ya mahindi na jamii ya kunde.
- Kutengeneza matrekta makongwe 8 Unguja na 4 Pemba na kununua jembe moja la kuchimbia na matatu ya kuburugia.
- Kupitia Program ya ASSP/ASDP-L kilimo cha maweni kutiliwa mkazo
- Mafunzo ya skuli za wakulima (farmer field schools) yataendelea kutolewa.

### 6.2.2 ELIMU KWA WAKULIMA

**Mheshimiwa Spika,** majukumu ya kitengo hiki ni kuelimisha, kushauri na kuunganisha matokeo ya utafiti kwa wazalishaji.

#### 6.2.2.1 UTEKELEZAJI WA MALENGO 2007/08

**Mheshimiwa Spika,** kitengo kimetekeleza yafuatayo:-

- Vipindi 20 vya Radio na 16 vya TV vilitayarishwa na kurushwa hewani.
- Wakulima 6,080 kutoka Wilaya zote za Unguja na Pemba wamepatiwa mafunzo juu ya usarifu na uhifadhi wa mazao ya mboga mboga na mizizi.
- Mafunzo ya utegenezaji, utumiaji na ulishaji wa jiwe la virutubisho kwa mifugo ya mbuzi na ngo'mbe wa maziwa yaliendelezwa.

- Mashirikiano na Taasisi zinazojihusisha na utoaji wa elimu kwa wakulima kama MVIWATA, ZAFFIDE, ZAZOSO yameimarika.
- Mabwana na mabibi shamba 130 walipatiwa mafunzo ya kuweka na kukopa, kukabiliana na maradhi na wadudu wa mimea, kufanya makisio ya mazao ya chakula, kilimo biashara (agro - business), mbinu za kukinga na kukabiliana na mafua ya ndege na maradhi mengine ya mifugo.

#### 6.2.2.2 MALENGO YA 2008/09

**Mheshimiwa Spika,** malengo ya Kitengo hiki ni kama yafuatayo:-

- Kuwaelimisha wazalishaji 1,200 juu ya mbinu za kilimo, mifugo na uvuvi.
- Kutoa mafunzo kwa mabibi /mabwana shamba 120 juu ya mbinu bora za kilimo na utafiti wa mazao ya chakula, biashara na ufugaji.
- Kuandaa ziara za wakulima na mabwana/mabibi shamba 10 ili kubadilishana utaalamu ikiwemo kuwapeleka katika maonesho ya nane nane Tanzania Bara.
- Kutayarisha na kuchapisha vipeperushi 3,000, vipindi vya redio 36 na TV 24 na kurushwa hewani.
- Kutoa taaluma za UKIMWI, mazingira na SACCOS.
- Kushajiisha wakulima 500 juu ya matumizi bora ya jembe la kukokotwa na ng'ombe na kuendelea kutoa mafunzo Unguja na Pemba.

### 6.2.3 HUDUMA ZA UTIBABU WA MIMEA

**Mheshimiwa Spika,** kitengo hiki kinatoa huduma na ushauri juu ya uhifadhi na utibabu wa mimea dhidi ya maradhi, wadudu na wanyama waharibifu wa mazao. Aidha, kitengo kinashughulikia huduma za karantini, ukaguzi wa mazao na upatikanaji wa madawa ya kuulia wadudu na magugu.

#### 6.2.3.1 UTEKELEZAJI WA MALENGO 2007/08

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa malengo ulikuwa kama ifuatavyo:-

- Ukaguzi wa bidhaa za kilimo zinazoingia na kutoka nchini umefanyika.
- Utafiti wa wadudu kwenye mazao ya mboga mboga na muhogo kwa kutumia madawa ya asili na mbolea ya vimelea vyenye manufaa ulifanyika. Utafiti huu umeonyesha kupungua kwa uharibifu wa wadudu hawa kwa asilimia 47.5
- Kemikali zenye thamani US$ 10,400 zimenunuliwa kupitia PADEP kwa ajili ya kufanya majaribio ya kudhibiti wadudu waharibifu wa matunda.
- Wakulima 268 walipatiwa mitego 546 ya kunasia nzi na kupatiwa mafunzo. Jumla ya nzi 2,041,114 walinaswa baada ya kugaiwa mitego hiyo ya majaribio kwa kipindi cha Agosti 2007 hadi April 2008.
- Mafunzo ya kudhibiti wadudu kwa mabwana na mabibi shamba 80 (Pemba 40 na Unguja 40) yamefanyika.

### 6.2.3.2 MALENGO 2008/09

**Mheshimiwa Spika,** kitengo kinakusudia kutekeleza yafuatayo:-

- Kuendeleza kazi za karantini na ukaguzi wa mimea.
- kuendelea kufanya utafiti na udhibiti wa wadudu waharibifu wa mimea pamoja na udhibiti wa nzi wa matunda kwa kutumia mitego ya kunasia nzi
- Kutoa ushauri wa kitaalamu na mafunzo kwa wakulima juu ya njia bora ya udhibiti wa wadudu waharibifu na maradhi ya mimea.
- Kuendeleza mashirikiano na taasisi nyengine za kimataifa katika kuyapatia ufumbuzi matatizo ya nzi wa matunda na "Spiral white flies"

### 6.2.4 CHUO CHA KILIMO KIZIMBANI.

**Mheshimiwa Spika,** Chuo hutoa mafunzo ya kilimo na mifugo katika ngazi ya cheti kwa miaka miwili kwa vijana waliomaliza kidato cha nne, vijana hao wanapomaliza masomo yao wanatarajiwa kufanya kazi kama mabwana/mabibi shamba. Aidha, vijana hao wanaweza kujiajiri wenyewe kwa kuanzisha miradi midogo midogo ya kilimo na mifugo. Pia chuo hutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wakulima na wafugaji juu ya mbinu bora za uzalishaji.

### 6.2.4.1 UTEKELEZAJI WA MALENGO 2007/08

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa malengo ulikuwa kama ifuatavyo:-

- Chuo kilifanikiwa kuchukuwa wanafunzi 61 kuanza masomo ya cheti, kati ya hao wanaume 17 na wanawake 44. Uamuzi wa kuchukua wanafunzi zaidi unatokana na watahiniwa wengi kufaulu katika usaili na wazee kukubali kuchangia gharama za chakula.
- Mafunzo ya muda mfupi ya ufugaji bora wa ng'mbe wa maziwa, kuimarisha malisho na kuchanganya vyakula vya mifugo yaliendelea kutolewa kwa wafugaji 30.

### 6.2.4.2 MALENGO 2008/09

**Mheshimiwa Spika,** Chuo kitatekeleza yafuatayo:

- Kuchukua wanafunzi 35
- Kuimarisha ekari 3 za malisho ya mifugo, kutunza mifugo ya ngo'mbe na mbuzi wa maziwa pamoja na kuku wa mayai na wanyama.
- Kuimarisha mazao kama muhogo, maharage, mboga mboga na miti ya matunda.
- Kuimarisha na kutoa mafunzo ya ukulima wa mboga mboga na vitunguu kwa wakulima vijana.

### 6.2.5 UTAFITI

**Mheshimiwa Spika,** Vituo vya Utafiti vinajukumu la kufanya utafiti wa mazao kwa lengo la kupata mbegu bora za mazao ya kilimo, zenye uwezo mkubwa wa kuzalisha kwa kutumia eneo dogo la ardhi, pamoja na kazi hizo kituo

kinaendelea kutoa huduma za maabara na maktaba(pongezi kwa watafiti wa mbegu).

### 6.2.5.1 UTEKELEZAJI WA MALENGO 2007/08

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa malengo ulikuwa kama ifuatavyo:-

- Miche ya migomba 100 na mbegu za muhogo kwa kutumia "meristem" na vitawi ambazo hazina maradhi imezalishwa na kuzisambaza kwa wakulima.
- Miti ya matunda; yenye sifa bora za uzalishaji ilizalishwa - milimau 1,050, miembe boribo aina ya muyuni miche 3,750, miembe juli 100, michungwa 2,500, mitofaa 800, midoriani 700, mishokishoki 2,000, midimu 2,000, na michenza 700.
- Mbegu mpya 100 za mpunga aina ya NERICA zimefanyiwa majaribio, 60 katika ardhi ya kilimo cha juu (upland) na 40 kilimo cha mabondeni (low land).
- Mbegu aina tano za muhogo Machui, Mahonda, Kizimbani, Kama na Mwari zilizalishwa kwa njia ya utafiti uliofanywa. Aidha mbegu za viazi vitamu zilifanyiwa utafiti nazo walipewa wakulima kwa kuzalisha mbegu zaidi ili ziweze kuwafikia wakulima wengi wa kilimo hicho.
- Mazao ya biashara yaliyozalishwa ni pamoja na mikungumanga 3,000; mihiliki 3,200; midalasini 1,700; tangawizi 1,500; manjano 2,000; vanilla 1,300; pilipili manga 2,500 na mibuni 300

### 6.2.5.2 MALENGO 2008/09

**Mheshimiwa Spika,** sekta ya utafiti imepanga kutekeleza yafuatayo:

- Kufanya utafiti wa kuzalisha miche ya migomba kwa kutumia viwango tofauti vya hormones.
- Kufanya utafiti wa udongo ili kupata viwango vya matumizi ya mbolea kwa mazao ya kilimo.
- Kufanya majaribio tofauti juu ya urutubishaji na utunzaji wa ardhi ya kilimo.
- Kuendeleza utafiti na uzalishaji wa mbegu bora za mazao ya biashara na chakula. Pamoja na uzalishaji miche ya mazao ya miti na matunda.
- Kukusanya mbegu tofauti za mpunga wa kienyeji na kuzihifadhi (Rice germplasm collection & maintenance) kwa kuziendeleza katika kituo cha utafiti, na kuendelea na utafiti wa mbegu za NERICA.

### 6.2.6 KITENGO CHA MINAZI

**Mheshimiwa Spika**, kitengo hiki kinajihusisha na kazi za utafiti wa wadudu waharibifu, uzalishaji wa mbegu bora zinazotokana na minazi ya kienyeji na kuhamasisha wakulima kuendeleza kilimo mchanganyiko pamoja na kuyafufua mashamba yao (rehabilitation) kwa upandaji upya wa minazi.

### 6.2.6.1 UTEKELEZAJI WA MALENGO 2007/08

**Mheshimiwa Spika;** sekta ya utafiti wa zao la nazi imetekeleza malengo yafuatayo:-

- Hekta 313 za mashamba ya minazi ya SMZ yaliendelezwa kutunzwa katika maeneo ya Kijichi, Bambi, Selem na Tumbe.
- Miche ya minazi 30,000 imezalishwa na tayari imetolewa kwa msimu huu wa masika.
- Mafunzo ya udhibiti wa wadudu Chonga na uimarishaji wa vitalu vya minazi yaliendeshwa kwa wakulima 387 wa Wilaya ya Kusini na Kaskazini

### 6.2.6.2 MALENGO 2008/09

**Mheshimiwa Spika;** sekta ya utafiti wa zao la nazi ina malengo yafuatayo:-

- Kufanya utafiti wa aina ya virutubisho muhimu vinavyohitajika kwa minazi.
- Kuendelea na utafiti wa kilimo bora cha minazi yenye kustahamili ukame, wadudu waharibifu na yenye uzazi mkubwa.
- Kuendelea na utafiti wa minazi chotara yenye muunganiko na minazi asilia.
- Kufanya ukusanyaji wa aina zote za minazi asilia inayopatikana hapa Zanzibar na kuihifadhi (germplasm collection).

### 6.2.7 MIRADI NA PROGRAMU

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2007/08, Kamisheni ya Kilimo, Utafiti na Elimu kwa Wakulima ilisimamia utekelezaji wa Mradi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji PADEP, kwa lengo la kuwajengea uwezo na kuwawezesha wakulima, wafugaji na wakulima wa mwani, ili waweze kuongeza kiwango cha uzalishaji wa mazao na hatimae kuongeza kipato. Maelezo ya kina ya mradi huu pamoja na utekelezaji wake yako katika (**Kiambatisho 6).**

### 6.2.8 MTAZAMO WA BAADAE

**Mheshimiwa Spika,** tafiti zilizopangwa kutekelezwa zitasaidia kupatikana kwa mbegu bora zenye kustahamili wadudu na maradhi na kutoa mazao mengi. Aidha, zitasaidia matumizi ya teknolojia bora katika kilimo hivyo kuhamasisha sekta ya watu binafsi kujiingiza katika kilimo na itasaidia wanawake na vijana wengi kushiriki katika kuendeleza kilimo. Hii itapelekea pato la mzalishaji kuongezeka na kuwa na uhakika wa chakula na lishe kama ilivyoainishwa katika MKUZA.

## 6.3 IDARA YA UMWAGILIAJI MAJI

**Mheshimiwa Spika,** Idara ina jukumu la kuendeleza na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji kama ilivyoainishwa katika Mpango Mkuu wa Umwagiliaji kwa lengo la kuongeza uzalishaji, uhakika wa chakula na kupunguza umasikini

nchini. Kazi zinazotekelezwa ni pamoja na kutoa ushauri kwa wakulima wa kilimo cha umwagiliaji, kutoa utaalamu katika masuala ya ujenzi na matumizi ya miundo mbinu ya umwagiliaji na kuimarisha jumuiya za wakulima wa kilimo cha umwagiliaji.

### 6.3.1 UTEKELEZAJI WA MALENGO 2007/08

**Mheshimiwa Spika,** Idara ilitekeleza malengo yafuatayo:

- Mita 1,900 za misingi mikuu ya umwagiliaji imejengwa kwa saruji sawa na asilimia 78 ya lengo. Ujenzi wa misingi ya Umwagiliaji kwa saruji umewezesha matumizi mazuri ya maji ambapo wakulima 350 wameongeza uzalishaji kwa kufaidika na maji hayo.
- Misingi ya kutolea maji 560m imejengwa katika kituo cha Ubago na kuwawezesha wakulima 75 kuongeza eneo la kilimo na mapato yatokanayo na kilimo
- Misingi ya ndani 800m imejengwa Weni na kuongeza ufanisi wa upatikanaji maji
- Ujenzi wa sakafu kwa zege katika vituo vya Mtwango na Weni umefanyika na kuleta matumaini kwa wakulima kuweza kuanika mpunga wao bila ya matatizo.
- Mabwawa ya Mipopooni na Weni yamefanyiwa ukarabati na hivyo kuwezesha maji kuvunwa na kutumika kwa kumwagilia na kuongeza uzalishaji.
- Ploti mpya 6.4ha katika kituo cha Mtwango zimetengenezwa na kuwezesha wakulima sitini (60) kupatiwa maeneo mapya ya kulima.
- Visima viwili vimechimbwa Tibirinzi na Cheju na visima vitatu vimekarabatiwa katika vituo vya Bumbwisudi, Kibokwa na Cheju, utekelezaji huu umewezesha kupatiwa maji wakulima 1,140 katika maeneo ya Bumbwisudi, Kibokwa na Cheju na kuongeza uzalishaji wa mpunga na mboga.
- Wakulima 3,600 wamepewa elimu na kuhamasishwa katika kilimo cha umwagiliaji na kutumia teknologia inayofaa ya uzalishaji wa mpunga na uendeshaji wa jumuiya za wakulima.
- Wafanyakazi wawili walipelekwa Kenya, wawili China na mmoja Korea kupata elimu katika shughuli za uvunaji wa maji ya mvua.
- Kitengo cha uvunaji maji ya mvua kimeanzishwa

### 6.3.2 MALENGO 2008/09

**Mheshimiwa Spika,** idara imelenga kutekeleza yafuatayo:

- Kuendeleza Mpango Mkuu wa Umwagiliaji Maji hekta 250
- Kuelimisha na kuhamasisha wakulima 4,000 katika kilimo cha umwagiliaji
- Kuendeleza mashamba madogo ya umwagiliaji Uzini na Mgenihaji hekta10, Matetema hekta 2 na Kitogani hekta 2 Kuendeleza kilimo cha uvunaji wa maji ya mvua (walengwa 175)

- Kuhamasisha umwagiliaji wa kutumia matone (drip irrigation) kwa kaya 40 katika hekta 40 kwa wilaya tisa ya Zanzibar
- Kuimarisha maghala ya mazao katika vituo vya umwagiliaji Cheju, Bumbwisudi, Mwera, Tibirinzi.

### 6.3.3 MTAZAMO WA BAADAE

**Mheshimiwa Spika;** Mtazamo wa baadae wa Idara ni kuweza kutekeleza Mpango Mkuu wa Umwagiliaji ambapo jumla ya hekta 2,000 ifikapo mwaka 2010 sawa na asilimia 23 ya eneo liloainishwa katika Mpango Mkuu wa Umwagiliaji Maji zitaweza kumwagiliwa na kulimwa kilimo cha mpunga na mboga mboga na hatimae kuongeza uzalishaji wa chakula na kupunguza umasikini.

### 6.3.4 MIRADI NA PROGRAMU ZA IDARA YA UMWAGILIAJI

**Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka huu wa fedha Idara ina Miradi miwili nayo ni:-

Mradi wa Mpango Mkuu wa Umwagiliaji Maji (**Kiambatisho 7)** na Mradi wa Mpango wa Kilimo cha Kisasa na Maendeleo ya Kilimo Cha Umwangiliaji Maji Tanzania **(Kiambatisho 8).**

### 6.4 IDARA YA MAENDELEO YA MIFUGO

**Mheshimiwa Spika,** Idara hii ina wajibu wa kupanga na kuratibu, maendeleo ya sekta ya mifugo na kutoa taaluma juu ya mbinu bora za uzalishaji mifugo ili kuufanya ufugaji uwe wa kibiashara na kuongeza mchango wake katika uchumi wa Taifa. Pia hutoa huduma ya matibabu na kinga kwa mifugo na husambaza mbegu bora za mifugo.

### 6.4.1 UTEKELEZAJI WA MALENGO 2007/08:

**Mheshimiwa Spika,** Idara ilitekeleza yafuatayo:-

- Vikundi 88 vya wafugaji vimeanzishwa na wafugaji 10,588 wanapatiwa ushauri na taaluma juu ya mbinu bora za ufugaji.
- Kupitia program ya ASDP-L, skuli 88 za wafugaji zimeanzishwa katika wilaya tisa za Unguja na Pemba.
- Kwa kutumia mbinu za ushajiishaji, Idara imetayarisha mafunzo, semina, vipeperushi, mabango, vipindi vya TV na redio kwa jamii ili watambue umuhimu wa kuikinga nchi yetu na maradhi ya miripuko. Wanafunzi 400, Masheha 70, wafugaji 180, wataalamu wa mifugo 20, wataalamu wa binadamu 20 wamepatiwa mafunzo kuhusu mafua makali ya ndege.
- Idara imeshajiisha wananchi na kuwapatia semina masheha na vikosi vya ulinzi juu ya udhibiti na uingizaji wa mifugo na bidhaa zake kinyume na sheria.

- Mifugo 176,510 ilipatiwa chanjo za kinga dhidi ya maradhi tofauti yakiwemo kichaa cha mbwa, chambavu, kimeta, vibuma, gumboro, na mahepe.
- Mifugo 227,519 ilitibiwa dhidi ya maradhi mbali mbali.
- Wafugaji 70 wamepatiwa taaluma na baadae kupewa mbegu za malisho kwa kupanda katika mashamba yao.
- Wafugaji 10,588 walitembelewa kwenye mashamba yao na kupewa taaluma juu ya ufugaji bora wa ng'ombe, kuku wa kienyeji, mbuzi wa maziwa na mifugo mingineyo.
- Kupitia programu ya ASDP-L, wafanyakazi 4 wamepatiwa mafunzo ya ziada katika kituo cha uzalishaji wa mbegu kwa kupandisha kwa njia ya sindano kituo cha Arusha na wawili nchini Kenya.
- Mitambo miwili ya uzalishaji nishati itokanayo na samadi ya ng'ombe imeanza kufanya kazi katika Mkoa wa Kaskazini na Mkoa wa Mjini-Magharibi. Aidha, taaluma hii itasambazwa kwa wafugaji wengine katika mikoa yote ya Unguja na Pemba.
- Mipango ya kufanyia mapitio sera ya mifugo inaendelea na kazi ya uwandishi wa sera hiyo inategemea kuanza hivi karibuni kwa kupitia programu ya ASPD-L.

### 6.4.2 MALENGO YA MWAKA 2008/09

**Mheshimiwa Spika**, Idara inalenga:-

- Kununua mtambo wa kutengeneza "Liquid nitrogen" ili kuendeleza huduma za upandishaji kwa sindano na kuzalisha ngombe bora wa maziwa kwa wananchi.
- Kutoa huduma za matibabu na kinga kwa mifugo na ushauri kwa lengo la kudhibiti maradhi ya mifugo nchini.
- Kuwashajiisha wananchi kufichua uingizaji wa mifugo na bidhaa zake kinyume na sheria ili kuzuia maradhi kutoka nje ya Zanzibar.
- Kujenga uwezo wa wataalamu na wafugaji ili waweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi.
- Kuwapatia taaluma wafanyakazi 40 ndani na nje ya nchi.
- Kusambaza taaluma na mitambo minane ya kutengeneza nishati itokanayo na kinyesi cha mifugo kwa wafugaji
- Idara itafanya matengenezo katika majengo machakavu ya Idara na kuweka vifaa vya kufanyia kazi.

### 6.4.3 MTAZAMO WA BAADAE

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na utekelezaji wa malengo ya Idara kwa mwaka wa fedha 2008/09, tunatarajia kuongezeka kwa idadi ya ngombe kutoka 188,442 hadi 193,242 kati yao kutakuwa na ongezeko la ng'ombe bora wa maziwa 560; kuthibiti uingiaji wa maradhi thakili ya mifugo kutoka nje ya Zanzibar; kutumika kwa nishati ya kinyesi cha ng'ombe kwa kupikia kutapunguza ukataji miti kwa kuni na mazingira yatahifadhika.

### 6.4.4 MIRADI NA PROGRAMU

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2008/09, Idara itatekeleza miradi miwili ambayo ni Mradi wa Kudhibiti Kichaa cha Mbwa na Mradi wa Upandishaji Ng'ombe kwa Sindano. Mradi wa kudhibiti Kichaa cha Mbwa una lengo la kudhibiti maradhi ya kichaa cha mbwa nchini kwa kuchanja mbwa wote wanao wasilishwa katika vituo vya kutoa chanjo mjini na vijijini na kuhasi mbwa wanaozurura na wale ambao wamiliki wake watakaoihitaji huduma hiyo. Mradi huu unaombewa jumla ya TShs. 10,000,000 kutoka SMZ. Aidha, Mradi wa Upandishaji Ngo'mbe kwa Sindano una lengo la kununua mtambo wa "liquid nitrogen" na kuzalisha mitamba bora ya ngo'mbe wa maziwa 560. Mradi unaombewa TShs. 508, 000,000 kutoka SMZ.

Kwa mwaka 2007/08 mtambo huo haukuweza kununuliwa kutokana na kupanda kwa bei kutoka shilingi 132,000,000 zilizotengwa hadi shilingi 508,000,000

## 6.5 IDARA YA MAZAO YA BIASHARA, MATUNDA NA MISITU

**Mheshimiwa Spika,** Idara hii ina majukumu ya kuwashirikisha wananchi kutunza na kuendeleza rasilimali za misitu na wanyama pori, kuhamasisha kilimo cha mazao ya biashara na kusimamia ukusanyaji wa mapato yatokanayo na mazao ya misitu.

### 6.5.1 UTEKELEZAJI WA MALENGO YA IDARA MWAKA 2007/08

**Mheshimiwa spik**a, utekelezaji wa malengo ya Idara ulikuwa kama ifuatavyo:

- Mpango wa Muda Mrefu wa Usimamizi wa Rasilimali za Misitu tayari umekamilika kwa kutolewa rasimu ya kwanza na kusambazwa kwa washirika
- Ujenzi wa banda la kupokelea wageni katika Hifadhi ya Taifa ya Jozani na Ghuba ya Chwaka umekamilika
- Mipango ya Makubaliano ya Usimamizi wa Maliasili za Misitu ya Jamii imekabidhiwa kwa shehia 10 zinazozunguka Msitu wa Hifadhi wa Kimaumbile Ngezi – Vumawimbi, Pemba
- Miche 35,000 ya minazi sawa na asilimia 70 ya lengo imeoteshwa katika vitalu vya uzalishaji
- Hekta 12 za mikoko zimepandwa katika Shehia ya Unguja Ukuu Kaepwani, hekta mbili Shehia ya Makoba Wilaya ya Kaskazini B na hekta 15 katika Shehia za Kisiwa Panza, Makombeni na Makoongwe. Aidha elimu ya uhifadhi wa mikoko imetolewa kwa Wilaya zote za Unguja na Pemba
- Doria 200 za mikoko zimefanyika katika Wilaya ya Kati na Mkoa wa Kaskazini – Unguja na Wilaya ya Micheweni na Mkoani – Pemba
- Kampeni ya upandaji miti kitaifa imefanyika katika mikoa yote ya Unguja na Pemba, jumla ya miti 40,000 ya misitu na matunda imepandwa

- Miche 1,200,000 ya misitu na matunda imezalishwa
- Utafiti na utekelezaji wa mapendekezo ya matumizi ya nishati mbadala umekamilika.

### 6.5.2 MALENGO YA IDARA 2008/09

**Mheshimiwa Spika,** Idara inalenga kutekeleza yafuatayo:

- Kutayarisha mipango ya usimamizi wa rasilimali za misitu katika shehia za Unguja Ukuu Kaepwani, Uzi na Ng'ambwa.
- Kutoa elimu ya uhifadhi wa misitu kwa wanajamii 200, mafunzo ya wafugaji nyuki 50, na kazi za mikono kwa wanafani 40
- Kufanya ukarabati wa majengo ya afisi na nyumba za wafanyakazi.
- Kuhamasisha wananchi katika kazi za upandaji miti kitaifa.
- Kuanzisha utalii wa Hifadhi ya Kiwengwa Pongwe, Msitu wa Hifadhi ya Kimaumbile wa Ngezi Vumawimbi na kuongeza njia za kupita watalii mpaka Wangwani katika Hifadhi ya Taifa ya Jozani na Ghuba ya Chwaka.
- Kufanya matayarisho ya mapitio ya Sera ya Misitu.
- Kushajiisha matumizi ya nishati mbadala na majiko sanifu

### 6.5.3 MTAZAMO WA BAADAE

**Mheshimiwa Spika**, Idara inategemea matokeo yafuatayo kutokana na malengo ya 2008/09 ya kuwa na mipango ya usimamizi wa rasilimali za misitu katika shehia za UngujaUkuu Kaepwani, Uzi na Ng'ambwa; kupungua kwa uharibifu wa misitu na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya misitu na asali, kuweka mazingira mazuri na endelevu ya hifadhi zetu ambayo yatasaidia kunyanyua sekta ya utalii wa kimaumbile na hivyo kuongeza mapato.

### 6.5.4 MIRADI NA PROGRAMU

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2008/09 Idara inasimamia miradi mikuu miwili ambayo ni:

- Mradi wa Uhifadhi wa Misitu na Maendeleo ya Jamii **(Kiambatisho 9)**
- Mradi wa Mpango wa Taifa wa Uimarishaji Mikarafuu (**Kiambatisho 10)**

## 6.6 IDARA YA UVUVI NA MAZAO YA BAHARINI

**Mheshimiwa Spika,** Idara hii ina majukumu ya kuwahudumia wavuvi, wakulima wa mwani pamoja na washirika wanaojishughulisha na uvuvi au mazao ya baharini ili kunyanyua hali zao kiuchumi. Jukumu jengine la Idara ni kuhakikisha utunzaji wa rasilimali na mazingira ya baharini kwa kuzingatia matumizi bora na endelevu ya rasilimali hizo. Idara pia inasimamia utekelezaji wa sheria na kanuni za uvuvi.

### 6.6.1 UTEKELEZAJI WA MALENGO 2007/08

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa malengo ulikuwa kama ifuatavyo:-

- Wakulima walipatiwa vifaa vya kulimia mwani vyenye thamani ya TShs. 17,600,000 vikiwemo boti moja ya kupakilia mwani na mashine yake, kamba 4,960 na taitai 2,475.
- Tani 8,485 za mwani (cottonii tani 63.8 na spinosum tani 8,421.2) zimezalishwa na kuwawezesha wananchi kujipatia Tsh 1, 321, 251,500.
- Wakulima wa mwani pia wamesaidiwa kwa kujengewa mabanda ya kuhifadhia mwani na kufugia kuku na mbuzi katika Shehia za Kilindi, Tumbatu Gomani na Jambiani Kibigija.
- Utafiti juu ya uwezekano wa kulima mwani cottonii kwenye kina kirefu cha maji unaendelea katika vijiji vya Bweleo na Kidoti. Utafiti huu ni shirikishi ambapo matokeo yake yatasambazwa kwa wakulima wa mwani
- Jumla ya Tsh 32, 357,500 zimetumika kwa ununuzi wa majokofu manne, boti moja ya uvuvi na mashine yake, vipande 60 vya nyavu za jarife na vifaa vyake, mishipi darzeni 288, ndoana boksi 54 pamoja na mfuko wa maafa kwa kamati za uvuvi.
- Ujenzi wa mabanda matatu ya kutumiwa na wavuvi wakati wa dago katika visiwa vya Pungume kwa Unguja (banda moja) na Misali kwa Pemba (mabanda mawili) pamoja na vyoo uliogharimu jumla ya TShs. 21,155,000 Aidha, TShs. 2,350,000 zimetumika katika ujenzi wa soko la kuuzia samaki Tumbatu
- Taaluma juu ya ufugaji wa samaki na chaza, ukuzaji wa kaa, pamoja na ukulima na uanikaji wa mwani zimetolewa kwa vijiji vya Unguja na Pemba.
- Idara imeendelea kufuatilia suala la kupatikana mwakilishi wa wakulima wa mwani na wavuvi katika Jumuiya ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima. Aidha, Idara inaendelea na kuwashajiisha wavuvi na wakulima wa mwani ili kuunda jumuiya za kitaifa za wavuvi na wakulima wa mwani kwa lengo la kujiunga na Jumuiya hiyo.
- Doria 72 za maji ya ndani zimefanywa kwa mashirikiano ya wanajamii na askari wa KMKM. Wavuvi 120 na vyombo vyao 30 walikamatwa kwa kutumia zana zinazokatazwa. Kati ya hao wavuvi wanne (4) wametiwa hatiani na kupewa adhabu zinazostahili kwa mujibu wa sheria. Aidha, mitego ya nyavu tisa na bunduki za kuvulia 42 zilichukuliwa na kuteketezwa, ambapo vyombo walirejeshewa wenyewe.
- Mitego 748 inayoharibu mazingira ikiwemo ya nyavu na bunduki imekabidhiwa Serikalini na kuchomwa moto.
- Doria 9 zimefanyika kwa kutumia ndege za kukodi na doria 2 za meli kwa mashirikiano na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika doria hizo meli 4 zilionekana zikivua kwa leseni halali zilizotolewa ama Zanzibar au Tanzania Bara.
- Elimu ya uhifadhi wa mazingira ya bahari, njia bora za uvuvi, ukulima wa mwani, utayarishaji wa sheria ndogo ndogo, pamoja na kuibua, kupanga na

kusimamia miradi imetolewa katika Shehia 127 zinazojishughulisha na uvuvi na 69 zinazolima mwani.

- Hatua ya kutayarisha kanuni chini ya sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu inaendelea.
- Zabuni kwa ajili ya michoro ya jengo la Afisi ya Mamlaka tayari imeshatangazwa.
- Sheria ya uanzishwaji ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu iko katika hatua za mwisho za utekelezaji wake.

### 6.6.2 MALENGO YA 2008/09

**Mheshimiwa Spika,** malengo ya Idara ni kama ifuatavyo:

- Kuendeleza kazi za uvuvi, kilimo cha mwani, kutoa nyenzo na taaluma kwa wavuvi na wakulima wa mwani.
- Kusimamia ujenzi wa Afisi na makao makuu ya Idara ya Uvuvi, Maeneo ya Hifadhi za Bahari na Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu.
- Kuanzisha na kusimamia maeneo mapya ya hifadhi za bahari za visiwa vya Changuu/Bawe, Tumbatu na Kojani.
- Kuendeleza kazi za doria katika maeneo ya maji (bahari) ya ndani.
- Kuwapatia mafunzo wafanyakazi wa Idara katika fani mbali mbali.
- Kuendelea kutoa elimu ya uhifadhi wa rasilimali za baharini na mazingira yake kwa jamii ya ukanda wa pwani na watumiaji wengine.
- Kuendeleza juhudi za kupatikana wajumbe wa kuziwakilisha jamii za wavuvi na wakulima wa mwani katika Jumuiya ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima.
- Kuendelea na kuwahamasisha wawekezaji katika sekta ya uvuvi.
- Kufanya marekebisho ya Sheria ya Uvuvi Nam. 8 ya mwaka 1988.

### 6.6.3 MTAZAMO WA BAADAE

**Mheshimiwa Spika,** mtazamo wa baadae ni kukuza ujuzi wa wavuvi na wakulima wa mwani na kuwapatia nyenzo ili kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao yanayozalishwa kwa lengo la kuinua kipato chao; kuwapatia wavuvi na wakulima wa mwani chombo kitakachoweza kusimamia maslahi yao kama vile kuwatafutia soko la bidhaa zao; kukuza mchango wa sekta ya uvuvi wa baharini na maji baridi (aquaculture) kwa Taifa (ajira, mapato na matumizi mazuri ya rasilimali); kuondoa uharibifu wa rasilimali na mazingira ya baharini; kuwawekea wafanyakazi mazingira mazuri ya kufanyia kazi; kutenganisha mamlaka ya usimamizi wa shughuli za uvuvi kati ya Idara na Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu. Aidha, kuweka mazingira mazuri ya usimamizi wa shughuli za uvuvi; kuongeza uzalishaji wa samaki katika maeneo ya uvuvi na kuishirikisha jamii katika usimamizi wa rasilimali na mazingira ya baharini na kuhakikisha upatikanaji endelevu wa rasilimali za baharini

### 6.6.4 MIRADI NA PROGRAMU

**Mheshimiwa Spika,** Idara ya Uvuvi na Mazao Baharini inatekeleza mradi mmoja mkubwa wa MACEMP unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. **(Kiambatisho 11)**

**Mheshimiwa Spika,** madhumuni ya mradi kwa maeneo tengefu ya Menai, MIMCA na PECCA kwa mwaka 2007/08 ilikuwa ni pamoja na kuendelea kutoa taaluma ya uhifadhi na ulinzi wa rasilimali za baharini kwa kushirikiana na wanajamii. Jamii ya ukanda wa pwani hivi sasa imepata mwamko mkubwa katika kulinda rasilimali za maeneo yao ya bahari. Katika mwaka 2007/08 maeneo hayo yaliombewa TShs. 34,000,000 kutoka Serikali na hadi kufikia Mei, 2008 jumla ya TShs. 20,000,000 zimepatikana ambazo ni sawa na asilimia 58.8. Kwa mwaka 2008/09 maeneo hayo ya jamii yanaombewa TShs. 20,000,000 kutoka Serikalini.

### 6.7 IDARA YA MAZINGIRA

**Mheshimiwa Spika,** Idara ina majukumu ya kushajiisha jamii juu ya uhifadhi wa mazingira ya ardhini, angani na majini, kutoa elimu ya mazingira na miongozo kwa jamii juu ya mbinu bora za kuhifadhi mazingira, pamoja na kuratibu tathmini za kimazingira kwa mipango, programmu na miradi ya maendeleo na vitega uchumi.

### 6.7.1 UTEKELEZAJI WA MALENGO YA 2007/08

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza malengo hayo, kazi zifuatazo zilifanyika:

- Jumla ya taarifa za miradi ya maendeleo 107 zilifanyiwa mapitio kwa nia ya kuangalia masuala ya mazingira na kutoa mapendekezo yaliyopelekea kutekelezwa kwa miradi hiyo bila ya kuathiri mazingira na jamii
- Maeneo 70 yanayotarajiwa kuanzishwa miradi ya vitega uchumi yalifanyiwa ukaguzi ili kuangalia kama yanafaa kimazingira
- Mikutano na Halmashauri za Wilaya pamoja na Mabaraza ya miji imefanyika na tayari kuna miradi midogo midogo ya uzoaji taka pamoja na kudhibiti maji machafu imeanzishwa kwenye maeneo hayo
- Idara kushirikiana na Bodi ya Madawa, Chakula na Vipodozi imeangamiza tani 40 za madawa ya hospitali yaliyomaliza muda wa matumizi.
- Kwa upande wa dhamana ya mazingira, dhamana hii imeanzishwa ila utekelezaji wake unahitaji nguvu za kisheria ambazo matayarisho yake yanaendelea
- Kutayarisha rasimu za Kanuni za upigwaji marufuku uingizaji na matumizi ya mifuko ya plastiki pamoja na kutayarisha Programu ya usafishaji wa taka za plastiki katika maeneo yote ya Unguja na Pemba.
- Kutayarisha programu ya kupunguza idadi ya kunguru Zanzibar.

### 6.7.2 MALENGO YA MWAKA 2008/09

**Mheshimiwa Spika,** Idara inalenga kutekeleza yafuatayo:

- Kuendeleza kazi za utoaji wa elimu ya mazingira kwa jamii na wawekezaji.
- Kufanya mapitio ya miradi pamoja na kuratibu tathmini za kimazingira kwa miradi ya maendeleo.
- Kufanya utafiti wa wanyama na miti inayopatikana katika visiwa vya Zanzibar.
- Kuendeleza kazi za uhifadhi wa kasa pamoja na kufanya utafiti juu ya mazingira ya maisha ya wanyama hao.
- Kusimamia upigwaji marufuku uingizwaji na matumizi ya mifuko ya plastiki baada ya kupitishwa kwa Kanuni hizo.
- Idara kupitia mradi wa Maji Machafu Chakechake kwa kushirikiana na Wilaya na Halmashauri itatengeneza mitaro ya maji machafu na ya mvua na kuyatia dawa kabla ya kumwagwa baharini.
- Kusimamia utekelezaji wa programu ya kupunguza idadi ya kunguru katika visiwa vya Unguja na Pemba.

### 6.7.3 MTAZAMO WA BAADAE

**Mheshimiwa Spika,** mtazamo wa baadae kwa Idara hii ni kuongeza kasi ya kuelimisha jamii juu ya uhifadhi wa mazingira, kushirikiana na jumuiya na mashirika mbali mali ya ndani na nje ya Zanzibar katika kutekeleza mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa duniani, na kutayarisha miongozo ya kimazingira itakakayoelekeza matumizi endelevu ya mazingira na maliasili zetu.

### 6.7.4 MIRADI NA PROGRAMU

**Mheshimiwa Spika,** Idara inatekeleza mradi wa Matumizi Endelevu ya Ardhi na Mazingira (SMOLE) kwa kushirikiana na Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi na Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani (MACEMP)

#### 6.7.4.1 Mradi wa Matumizi Endelevu ya Ardhi na Mazingira (SMOLE)

**Mheshimiwa Spika,** madhumuni ya mradi huu ni kuandaa mpango wa muda mrefu wa kusimamia matumizi endelevu ya ardhi na mazingira na kujenga uwezo wa Idara katika kusimamia masuala ya ardhi na mazingira ili kuleta maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii.

#### 6.7.4.2 UTEKELEZAJI WA MALENGO YA 2007/08

**Mheshimiwa Spika,** mradi ulitekeleza malengo yafuatayo:

- Kuratibu mapitio ya Sera ya taifa ya Mazingira na hivi sasa yako katika hatua za mwisho.

- Kuwapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi wa Idara ya Mazingira katika fani za teknolojia ya habari na mawasiliano, elimu ya mazingira, rasilimali watu Accounting, computer na ICM.
- Kuratibu usimamizi wa tathimini za kijamii na kimazingira
- Kutayarisha mabango 1,500 za kuelimisha jamii ambazo zilihusiana na hatari za matumizi ya mifuko ya plastiki na uchimbaji wa mawe Kisiwani Pemba. Posta hizo zimesambazwa kwenye taasisi za Serikali pamoja na taasisi nyengine.
- Kutayarisha nakala 1,000 za kalenda ya mwaka 2008 na kusambazwa kwa washirika wa sekta ya mazingira.
- Kutayarisha vipindi 12 vya radio na 8 vya TV. Vipindi vyote hivyo vimetayarishwa kwa nia ya kuhamasisha na kuelimisha jamii juu ya hifadhi ya mazingira.
- Kuandaa ripoti ya awali ya viwango vya mazingira (Environmental Standards) vya maji machafu yanayotoka majumbani na viwandani.

### 6.7.4.3 MALENGO YA 2008/09

**Mheshimiwa Spika,** mradi unalenga kutekeleza yafuatayo:

- Kukamilisha kazi za mapitio ya Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1992.
- Kweka miongozo ya usimamizi wa matumizi ya maliasili zisizorejesheka.
- Kuendelea kujenga uwezo wa wafanyakazi kwa kuwapa mafunzo pamoja na ununuzi wa vitendea kazi
- Kuendelea kufanya utafiti wa hali ya bioanuwai ya Zanzibar.
- Kukamilisha kazi ya kutayarisha viwango vya kitaifa vya kimazingira.

### 6.7.4.4 Mradi wa Usimamizi wa mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani (MACEMP)

**Mheshimiwa Spika,** Idara inatekeleza baadhi ya vipengele vya Mradi wa MACEMP unaoratibiwa na Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini. Vipengele hivyo ni pamoja na Tathmini za Athari za Kimazingira na Jamii na kuendeleza Mpango wa Uwiano wa Usimamizi wa Rasilimali za Pwani.

### 6.7.4.5 UTEKELEZAJI WA MALENGO YA 2007/08

**Mheshimiwa Spika,** mradi umetekeleza malengo yafuatayo:

- Kuendesha mafunzo kwa wafanyakazi 50 wa Idara juu ya Tathmini za Athari za Kimazingira kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Hifadhi ya Mazingira (NEMC).
- Kufanya zoezi la ufuatiliaji (monitoring) katika hoteli zote za kitalii za Unguja na Pemba ambapo jumla ya miradi ya hoteli 138, Unguja 123 na Pemba 15 ilifanyiwa ukaguzi na wahusika kupatiwa ushauri mwafaka wa kimazingira.

- Kuendesha kampeni za usafi wa mazingira kwa wananchi wa Shehia za Bububu, Kibweni, Mwanyanya, Sharifumsa, Kwahani, Kwaalinato, Matarumbeta na Sogea.
- Kuendesha mafunzo ya mazingira kwa wananchi wa wilaya zote za Pemba, pamoja na kutathmini uharibifu wa mazingira kwa maeneo yanayoingia maji ya bahari katika Kisiwa cha Kojani na kijiji cha Mwambe, Pemba.
- Kuainisha maeneo yanayohitaji kufanyiwa marekebisho kwa Sheria ya Mazingira ya mwaka 1996.

### 6.7.4.6 MALENGO YA 2008/09

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa MACEMP kupitia Idara ya Mazingira umepanga kutekeleza yafuatayo:

- Kukamilisha mapitio ya Sheria ya Mazingira ya mwaka 1996.
- Kukamilisha matayarisho ya mikakati ya kitaifa ya Usimamizi wenye uwiano wa maeneo ya pwani (ICM Action Plan).
- Kuendeleza ufuatiliaji wa hali ya mazingira katika miradi ya hoteli za kitalii za ukanda wa pwani Unguja na Pemba.
- Kuratibu usimamizi wa tathmini za kijamii na kimazingira.
- Kushughulikia maeneo ya mmong'onyoko wa fukwe
- Kutia dawa michirizi ya maji machafu (sewage)

## 6.8 IDARA YA VYAMA VYA USHIRIKA

**Mheshimiwa Spika,** Idara ina majukumu ya kuhamasisha uanzishwaji wa vyama vya ushirika na kuvisajili kisheria, kutoa elimu ya ushirika kwa vyama vya ushirika, kufanya ukaguzi wa kawaida, ukaguzi wa mahesabu pamoja na kukusanya mapato ya ukaguzi na usajili wa vyama vya ushirika. Aidha, Idara inasimamia utekelezaji wa sheria ya ushirika na kutoa ushauri na miongozo mbali mbali kwa vyama vya ushirika na kusuluhisha migogoro inayojitokeza katika vyama vya ushirika.

### 6.8.1 UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MWAKA 2007/08

**Mheshimiwa Spika,** Idara imetekeleza malengo yake kama ifuatavyo:-

- Jumla ya vyama 189 vya Ushirika vimesajiliwa Unguja na Pemba, kati ya hivyo 101 ni vya SACCOS na 88 vya uzalishaji mali.
- Idara tayari imetayarisha rasimu ya Sera ya Ushirika ya Zanzibar.
- Vyama 335 vya Ushirika vimeweza kuchunguzwa na kufungiwa mahesabu katika Unguja na Pemba.
- Wanaushirika 13,790 wa vyama vya Ushirika vya Akiba na mikopo (SACCOS) na vya uzalishaji mali wamepatiwa taaluma.
- Vipindi 20 vya redio vya elimu ya Ushirika vilirushwa hewani kupitia Sauti ya Tanzania Zanzibar

- Kupitia mradi wa ASSP/ASDP-L Idara imepata gari moja na pikipiki moja kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake.

### 6.8.2 MALENGO YA 2008/09

**Mheshimiwa Spika,** Idara inalenga yafuatayo:-

- Kushajiisha na kuhamasisha wananchi waweze kuanzisha vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa na Vyama vya Uzalishaji Mali
- Kuendelea na zoezi la kuanzisha Sera ya Ushirika na kufanya mabadiliko ya Sheria ya Ushirika.
- Kuchunguza na kukagua mahesabu ya vyama vya ushirika 120 katika Wilaya za Unguja na Pemba na kutoa ushauri wa kitaalamu
- Kuwapatia mafunzo ya kitalamu wafanyakazi wa Idara
- Kuendelea kuwajengea uwezo wanaushirika kwa kuwpatia ujuzi wa kitaalamu
- Kushirikiana na taasisi mbali mbali za kiserikali na zisizo za kiserikali (NGO's) zenye mwelekeo wa kuleta maendeleo ya ushirika nchini.

### 6.8.3 MTAZAMO WA BAADAE

**Mheshimiwa Spika,** mtazamo wa baadae wa Idara ni kuwa na SACCOS endelevu, zinazomilikiwa na wanachama wenyewe zenye mtaji mkubwa unaotokana na nguvu za wanachama wenyewe, kujenga mazingira mazuri yanayohusiana na uanzishaji na uendeshaji wa vyama vya ushirika vya kiuchumi na vitakavyotoa ajira ya kudumu kwa wananchi. Pamoja na hayo Idara inatarajia kuwasilisha rasimu Sera ya Ushirika kwa washiriki wa maendeleo hivi sasa.

## 6.9 KARAKANA YA MATREKTA

**Mheshimiwa Spika,** Karakana ya Matrekta inatoa huduma za kiufundi ikiwa ni pamoja na kutengeneza matrekta, gari pamoja na kufanya kazi za uchongaji na uchomaji.

### 6.9.1 UTEKELEZAJI WA MALENGO 2007/08

**Mheshimiwa Spika,** Karakana imetekeleza malengo yafuatayo:-

- Matrekta 12 ya Kilimo yametengenezwa, manne Pemba na manane Unguja sawa na asilimia 48 ya lengo.
- Ukodishaji wa matrekta kwa kazi za ukulima haukufanyika kutokana na trekta lilopangiwa kazi hiyo kuharibika.
- Mafunzo ya vitendo yaliendelea kutolewa.

### 6.9.2 MALENGO KWA MWAKA 2008/09

**Mheshimiwa Spika**, Karakana inategemea kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kutengeneza na kuyahudumia matrekta 17 ya Serikali ikijumuisha na matrekta 12 mapya pamoja na kutengeneza matrekta ya miradi na ya watu binafsi.
- Kukodisha matrekta mawili kwa kazi za ukulima.

- Kutoa huduma za uchongaji na uchomaji.
- Kuendelea kutoa mafunzo ya vitendo kwa vijana kutoka taasisi za Serikali na za watu binafsi.

## 7.0 MATATIZO NA CHANGAMOTO YA SEKTA YA KILIMO

7.1 **Mheshimiwa Spika,** pamoja na jitihada kubwa zinazochukuliwa na Serikali, Sekta ya Kilimo bado inakabiliwa na matatizo na changamoto zinazosababisha kupungua uzalishaji. Miongoni mwa hayo ni pamoja na uhaba wa vitendea kazi**,** uchakavu na ufinyu wa majengo na taasisi za Wizara. Pia tatizo la wanyama waharibifu na wizi wa mazao na mifugo bado linaendelea kuwa sugu, kuzuka mara kwa mara kwa maradhi ya miripuko, matumizi ya pamoja (multi-use) kati ya wavuvi na watalii ndani ya maeneo ya hifadhi za bahari, uharibifu wa mazingira na matumizi mabaya ya maliasili.

7.2 **Mheshimiwa Spika,** changamoto na matatizo mengine ni pamoja na maeneo mazuri ya uzalishaji kutumika kwa ujenzi, uvamizi wa maeneo ya kilimo na misitu ya serikali, uwekezaji mdogo katika sekta ya kilimo na mabadiliko ya hali ya hewa yanayopelekea mvua zisizotabirika. Aidha, ukosefu wa huduma za mikopo kwa wakulima, kuongezeka kwa gharama za uzalishaji ikiwemo huduma za pembejeo na matrekta, bei ndogo ya mazao ya kilimo hasa mwani, matumizi hafifu ya teknolojia na utaalamu katika Sekta ya Kilimo, na kilimo cha kutegemea mvua.

## 8.0 MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI

8.1 **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi kinachomalizikia tarehe 30 Juni, 2008. Wizara hii ilikadiria kukusanya mapato ya TShs. 696,080,000 kutokana na vyanzo vyake, mpaka kufikia Aprili, 2007. Wizara ilikusanya mapato ya Tshs 399,843,684 ambazo ni sawa na asilimia 57 ya makadirio. Mpaka mwisho wa mwezi wa Juni, 2008 Wizara inakadiriwa kukusanya jumla ya TShs. 75,000,000 na kufanya jumla ya makusanyo kuwa TShs. 474,843684 Kwa hivyo mafanikio ya ukusanyaji wa mapato yatafikia asilimia 68. (**Kiambatisho 12).**

8.2 **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2007/08, Wizara ilitengewa jumla ya TShs. 997,313,000 kwa kazi za maendeleo kwa kukimu miradi 12. Fedha zilizotolewa kwa kazi za maendeleo mpaka kufikia Aprili, 2008 ni TShs. 538,856,131.25 ambazo ni sawa na asilimia 54 (**Kiambatisho 13)**. Aidha kwa mwaka wa fedha 2007/08 makadirio ya matumizi yalikuwa TShs. 5,941,200,000 kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Aprili 2008 fedha zilizotolewa ni TShs. 4,277,295,077.05 sawa na asilimia 72

8.3 **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2008/09 Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira inakadiriwa kukusanya mapato ya TShs. 696,702,000 kutokana na

vianzio vyake. Kwa upande wa matumizi Wizara ina miradi 15 na inatarajia kutumia TShs. 19,888,723,000 kwa kazi za maendeleo ikiwa TShs. 1,300,000,000 ni mchango wa SMZ na Jumla ya TShs. 18,588,723,000 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kazi za kawaida, Wizara ya Kilimo inatarajia kutumia TShs. 6,481,000,000.

## 9.0 HITIMISHO

9.1 **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuzishukuru Serikali za nchi zifuatazo – Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Egypt, Afrika ya Kusini, China, Jamhuri ya Korea, Japan, India, Iran, Israel, Finland, Uholanzi, Austria, Australia, Cuba, USA, UK. Aidha, napenda kuwashukuru washirika wa kimaendeleo wakiwemo FAO, WB, IFAD, ADB, KOICA, JICA, USAID, UNDP, WSPA, WFP, WWF, IAEA,FFI, WCS , ACTION AID, GLOBAL FUND, IDA, UNICEF, DANIDA, Chuo Kikuu cha Turku (Finland). Pia tunazishukuru Jumuiya za EAC, EU, SADC, AU FARM AFRICA Rockfeller Foundation. Aidha, tunazishukuru Wizara za SMZ na taasisi za Serikali na zisizo za kiserikali zinazosaidia kuleta maendeleo ya Sekta ya Kilimo.


9.2 **Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Naibu Waziri Mheshimiwa Khatib Suleiman, Katibu Mkuu Nd. Rahma Mshangama, Naibu Katibu Mkuu Nd. Ali Khamis Makarani, Makamishna na Wakurugenzi, wataalamu na wafanyakazi wote wa Wizara Unguja na Pemba kwa kazi zao nzuri na zenye ufanisi wa hali ya juu. Aidha, nawapongeza Wakuu wa Mikoa, wakulima, wafugaji, wavuvi, wanamazingira na washirika wote kwa kazi zao nzuri za kuleta maendeleo katika Sekta ya Kilimo. Aidha navipongeza vyombo vyote vya habari kwa utoaji wa habari za sekta ya kilimo.

9.3 **Mheshimiwa Spika,** sasa nawaomba waheshimiwa wajumbe wa Baraza lako Tukufu wayapokee, wayajadili, watupe ushauri, maoni na kutuelekeza na hatimae kupitisha makadirio na kuidhinisha jumla ya TShs. 26,369,723,000 ambazo TShs. 19,888,723,000 ni kwa kazi za maendeleo na TShs. 6,481,000,000 kwa kazi za kawaida. Pia naomba idhini ya kukusanya mapato ya TShs. 696,702,000 kwa mwaka wa fedha 2008/09.

9.4 **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**MHE. BURHAN SAADAT HAJI (MBM)**
**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA MAZINGIRA**
**<u>ZANZIBAR</u>**

**KIAMBATISHO Na. 1: MWENENDO WA MVUA UNGUJA NA PEMBA.**



**KIAMBATISHO Na. 2. TAKWIMU ZA UZALISHAJI WA MAZAO KWA MWAKA 2006/2007**

| | ZAO | UZALISHAJI MWAKA 2006 TANI | UZALISHAJI MWAKA 2007 TANI | TOFAUTI YA UZALISHAJI 2006/07 TANI | TOFAUTI KWA ASILIMIA2006/07 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Muhogo | 190,266 | 187,213 | -3,053 | -2 |
| 2 | Migomba | 88,438 | 93,641 | 5,203 | 6 |
| 3 | V/Vidogo | 63,949 | 45,620.28 | -18,329 | -29 |
| 4 | V/Vikuu | 5,100 | 8,192.36 | 3,092 | 61 |
| 5 | Mpunga | 24,730 | 20,037.64 | -4,692 | -19 |
| 6 | J/ Kunde | 683 | 1,029.20 | 346 | 51 |
| 7 | Mahindi | 3,927 | 1,930.50 | -1,997 | -51 |
| 8 | N.Nyasa | 93 | 75.8 | -17 | -18 |
| 9 | Mboga | 5,787 | 3,824.28 | -1,963 | -34 |
| 10 | Maboga | 600 | 1,154.50 | 555 | 92 |
| 11 | Mtama | 409 | 794 | 385 | 94 |
| | **JUMLA** | **383,982** | **363,513** | **-20,469** | **-5** |

**KIAMBATISHO Na. 3. PROGRAMU YA KUENDELEZA HUDUMA ZA KILIMO (ASSP)**

| |
|---|
| **Maelezo mafupi ya mradi:**<br>Programu hii imeanza Januari 2006 ikiwa na madhumuni ya kuwawezesha wakulima kupata na kutumia utaalamu na teknolojia za kilimo ambazo zitaongeza uzalishaji na kumuongezea mkulima kipato na uhakika wa chakula. Programu inalenga kujenga mashirikiano kati ya taasisi za umma na za watu binafsi katika kutoa huduma bora kwa wakulima. Aidha program itaimarisha mfumo wa habari za masoko, na kuongeza uwezo wa upatikanaji wa pembejeo. Programu inatekelezwa katika Wilaya tisa za Unguja na Pemba ikianzia na Shehia kumi kwa kila wilaya. |
| **Gharama**: USD 5.9 million sawa na Shillingi billion 7.1 |
| **Wachangiaji**: SMZ (22%), IFAD (77.1%), Walenga (0.7%) |
| **Lengo Kuu**: Kuinua hali ya maisha ya wakulima kwa kuongeza uzalishaji wenye tija, kuongeza kipato, uhakika wa chakula na kupunguza umaskini. |
| **Malengo Maalum**:<br>1. Kuwawezesha wakulima maskini na wanawake kuzitumia taaluma na teknologia za kisasa za kilmo zitakazo tolewa na watoa huduma kwa lengo la kuongeza uzalishaji na tija.<br>2. Kuweka mfumo wa utatibu na udhibiti wa viwango vya huduma. |
| **Vipengele vya Programu**:<br>1) Kuwawezesha wakulima, 2) Kutoa huduma za kilimo, 3) Uratibu na uendeshaji wa programu. |
| **Bajeti ya mwaka 2007/2008:**<br>1.Jumla: TSh 3,002,138,000 2. IFAD:Tsh 2,722,834,000, 3. SMZ: TSh 279,304,000, 4. Walengwa Tsh. 18,700,000 |
| **Utekelezaji 2007/2008:**<br>1. Vikundi 216 vimeanzishwa na kupewa mafunzo ya aina mbali mbali kulingana na mahitaji yao, ziara baina ya vikundi bado hazijaanza.<br>**2.** Upembuzi shirikishi umefanyika katika Shehia 54.<br>3. Katika kuwajenga uwezo wakulima, shughuli zifuatazo zimefanyika:<br>a) Mtaala wa skuli za wakulima umetayarishwa<br>b) Mafunzo yametolewa kwa walimu wa walimu katika kuendesha skuli za wakulima<br>c) Mafunzo yametolewa kwa wawezeshaji wa skuli za wakulima<br>4. Matayarisho ya awali ya kusaidia bodi za kuratibu kazi za utafiti na elimu kwa wakulima yameanza.<br>**5.** Mafunzo ya muda mfupi na mrefu yametolewa kwa wafanyakazi 12 katika ngazi zifuatazo: Shahada ya juu 3, shahada 3 na stashahada 6, na wafanyakazi 3 wamepata mafunzo mafupi nchini Swaziland na mmoja Nairobi. Warsha juu ya uzalishaji mbegu na utafiti wa mpunga zimefanyika Unguja na Pemba. Ziara ya kimafunzo ilifanyika Dodoma ambapo wakulima tisa kutoka katika vikungi 3 vya SACCOS Bambi waliwatembelea wenzao ili kujifunza na kubadilishana mawazo juu ya uendeshaji wa vikundi vya kuweka na kukopa. |
| **Bajeti ya mwaka 2008/2009**<br>Programu inatarajia kutumia jumla ya TShs 2,818,916,006, IFAD Tshs. 2,171,851,384, SMZ Tsh. 628,135,052 na walengwa Tshs. 18,929,570 |
| **MALENGO YA Mwaka 2009/2008**<br>1. Kuendelea kufanya upembuzi shirikishi katika Shehia mbali mbali<br>2. Kuendelea kuvipa elimu vikundi vya skuli za wakulima na kuanzisha mpya 180<br>3. Kuwapa mafunzo ya muda mfupi na mrefu wafanyakazi wa Wizara ya Kilimo<br>4. Kuandaa ziara za kimafunzo ndani ya Zanzibar na Tanzania Bara<br>5. Kusaidia shughuli za utafiti na elimu kwa wakulima. |

**KIAMBATISHO Na. 4 PROGRAMU YA KUENDELEZA HUDUMA ZA-MIFUGO (ASDP- L)**

| |
|---|
| **Maelezo mafupi ya mradi:**<br>Programu hii imeanza Januari 2006 ikiwa na madhumuni ya kuwawezesha na kuwaendeleza wafugaji maskini ili kuinua hali yao ya kipato na kuwaondoshea umaskini. Programu inatekelezwa katika Wilaya tisa za Unguja na Pemba ikianzia na shehia kumi kwa kila wilaya. |
| **Gharama**: USD 3.76 million |
| **Wachangiaji**: SMZ (6.1%), IFAD (93%), Walenga (0.9%) |
| **Lengo Kuu**: 1.Kupunguza umasikini, kuongeza uhakika wa chakula, kuongeza kipato cha watu masikini wanaotegemea mifugo katika maisha yao. |
| **Malengo Maalum**:<br>1. Kuimarisha hali ya maisha ya wafugaji walio masikini<br>2. Kuimarisha uwezo wa kiutawala na kiutendaji wa Jumuiya za wafugaji.<br>3. Kuimarisha utoaji wa huduma za mifugo kwa wafugaji wadogo wadogo<br>4. Kuimarisha huduma za miundo mbinu ya masoko kwa bidhaa za mifugo<br>5. Kuimarisha uwezo wa taasisi za kitaifa na za kiwilaya katika kutoa huduma bora kwa sekta ya mifugo |
| **Vipengele vya Programme**:<br>1) Kuwawezesha wafugaji, 2) Kusaidia maendeleo ya sekta ya mifugo, 3) Mijadala ya Sera na marekebisho ya Sheria, 4) Uratibu wa Programu. |
| **Bajeti ya mwaka 2007/2008:**<br>1. Jumla: TSh 2, 144, 800,000 2. IFAD:Tsh 2,050,736,000, 3. SMZ: TSh 94,064,000, 4. Walengwa Tsh. 15,300,000 |
| **Utekelezaji 2007/2008:**<br>Malengo hayakutekelezwa, bado yapo kwenye mchakato wa taratibu za ununuzi (procurement procedures). |
| **Bajeti ya mwaka 2008/2009**<br>**1. Jumla Tshs. 1,896,153,000 2. IFAD Tshs. 1,743,029,373. SMZ Tshs.136,572,549 3. Walengwa Tshs. 16,551,078.** |
| **MALENGO YA Mwaka 2008/2009**<br>1.Kufanya utafiti wa matatizo ya wafugaji<br>2. Kutambua huduma zinazohitajika ili kuwawezesha wafugaji kuongeza uzalishaji na kuzalisha kibiashara<br>3. Kufanya utafiti wa mfumo wa uzalishaji wa mifugo (kuku, ng'ombe na wanyama wadogo wadogo.<br>4. Kufanya ukarabati wa vituo na maabara za mifugo<br>5. Kuwapa mafunzo watoa huduma za msingi za mifugo kutoka Shehia mbali mbali |

**KIAMBATISHO Na. 5 PROGRAMU YA UHAKIKA WA CHAKULA NA LISHE**

| |
|---|
| **Maelezo mafupi ya Programu**:<br>Programu ya Uhakika wa Chakula na Lishe imeandaliwa sambamba na Sera ili kuwa na Mpango toshelevu na unaohusisha sekta na wadau wote katika ngazi za utekelezaji wa Malengo ya kukabiliana na kutokuwa na Uhakika wa Chakula na Lishe kama yalivyoelekezwa na MKUZA na Sera ya Taifa ya Uhakika wa Chakula na Lishe. Programu hii imebuniwa kwa kuzingatia haja ya kusaidiana na juhudi zilizopo za kupunguza umasikini na kutokuwa na Uhakika wa Chakula na hivyo inaelekeza kazi na hatua muhimu kwa sekta ya Kilimo na sekta nyenginezo katika kutatua matatizo ya kutokuwa na Uhakika wa Chakula na Utapiamlo |
| **Maeneo ya Programu:** Utekelezaji utafanyika katika Wilaya zote kumi za Unguja na Pemba |
| **Muda wa Programu**: Miaka 10 itakayotekelezwa katika vipindi viwili vya miaka mitano mitano kuanzia Julai 2008 |
| **Gharama**: USD 15 million katika awamu ya miaka mitano ya mwanzo |
| **Wachangiaji**: SMZ, FAO, UNICEF,WFP,UNDP na Washirika wengine wa Maendeleo |
| **Lengo Kuu:**<br>Lengo kuu la Programu ni kuchangia katika hatua za kitaifa za kupunguza umasikini na njaa, kukabiliana na hali ya kutokuwa na uhakika wa chakula na lishe katika ngazi za Taifa, Jamii na Kaya na kushajiisha ushirikiano wa jamii katika hatua za kujiongezea kipato, kuondoa njaa na kufikia hali ya kila mtu ya kuwa na haki ya kula na kushiba |
| **Malengo Maalum**<br>▪ Kuongeza kasi ya upatikanaji wa chakula kwa kuzidisha uzalishaji wa chakula wa ndani ya nchi<br>▪ Kuongeza uwezo wa wananchi hasa wa kipato cha chini wa kupata chakula;<br>▪ Kuboresha matumizi sahihi ya chakula bora na salama kwa wanafamilia;<br>▪ Kupunguza hali tete ya kutokuwa na uhakika wa chakula kwa jamii isiyo na uhakika wa kupata chakula na kuweka mikakati thabiti kwa ajili ya kutoa hifadhi kwa jamii na kulifanya taifa kuweza kujiweka tayari na majanga kama haya ya upungufu wa chakula;<br>▪ Kuhakikisha kuwa masuala ya Uhakika wa Chakula na Lishe yanazingatiwa katika sera za sekta nyengine zinazohusika ili kuwa na mwelekeo mmoja kitaifa.<br>▪ Kuongeza ufanisi wa masoko ,biashara na upatikanaji mikopo nafuu kwa miradi midogo midogo na ya kati na kwa wakulima wadogo wadogo<br>▪ Kuimarisha na kujenga uwezo wa taasisi zinazosimamia masuala ya uhakika wa chakula na lishe<br>▪ Kuanzisha na kuwezesha mfumo makini wa uratibu na uongozi wa kazi za uhakika wa chakula na lishe. |
| **Vipengele vya Programu**<br>1. Miradi ya Jamii ya kuendeleza Uhakika wa Chakula na Lishe<br>2. Uwezeshaji wa Uhakika wa Lishe na Kukabiliana na upungufu wa Chakula kutokana na Maafa.<br>3. Kuwezesha Mazingira mazuri ya Utekelezaji wa Sera ya Uhakika wa Chakula na Lishe<br>4. Uratibu na Uongozi wa Programu. |
| **Gharama mwaka 2008/2009** |

| |
|---|
| Programu inaombewa Tzs 74,000,000 kutoka SMZ na inatarajia kutumia USD 366,000 kutoka FAO kupitia UN- Joint Programme 5 |
| **Malengo ya mwaka 2008/2009**<br>• Kutengeneza rasimu ya sheria itayopelekea kuundwa na kufanyakazi kwa Divisheni ya Uhakika wa Chakula na Lishe ndani ya Wizara ya Kilimo ambayo itakuwa na jukumu la kuratibu utekelezaji wa Sera na Programu ya Uhakika wa Chakula na Lishe<br>• Improved food availability by enhancing domestic food production through facilitation of Farmer Field<br>• Strengthen H/H and community support structure and mechanism to ensure H/H food security and nutrition for vulnerable groups<br>• Facilitate formulation of Agricultural Marketing Policy and Strategy through relevant studies to inform the process and provide policy advise<br>• Develop PM&E framework to monitor the implementation of FSN Programme<br>• Kuhamasisha uelewa wa Sera na Programu ya Uhakika wa Chakula na Lishe katika ngazi za Taifa, Wilaya na Jamii.<br>• Kujenga uwezo wa Wilaya na Jamii kupanga mipango ya maendeleo inayozingatia suala la Uhakika wa Chakula na Lishe. |

**KIAMBATISHO Na. 6. MRADI SHIRIKISHI WA MAENDELEO YA KILIMO NA UWEZESHAJI (PADEP)**

| **MRADI WA PADEP** |
|---|
| Maelezo mafupi ya Mradi:<br>Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji PADEP ni Mradi wa miaka mitano ulioanza Tarehe 28 Agosti 2003. Madhumuni ya Mradi huu ni kukuza maendeleo ya kilimo kwa kutoa kipaumbele utumiaji wa teknolojia zinazofaa hasa kwa walengwa na kuiwezesha sekta binafsi kushiriki katika kuboresha soko la pembejeo za kilimo na mazao yanayotokana na kilimo. |
| **Maeneo ya Mradi:** mradi unatekelezwa katika shehia 94 (Unguja 67 na Pemba 27) za Wilaya tano (3 Unguja na 2 Pemba) na itanufaisha kaya 7,520. |
| **Muda ya Mradi:** Miaka mitano |
| **Gharama:** US $ 4.362 million |
| **Wachangiaji:** 1. IDA: US $ 3.5 million 2. SMZ na Walengwa: US $ 0.862 million |
| **Lengo kuu:** kuwajengea wakulima uwezo wa kitaalamu katika kutambua matatizo yao na kuibua miradi yao kwa lengo la kuongeza uzalishaji na tija na kushajiisha sekta binafsi kushiriki katika kutoa huduma za kilimo. Aidha kuongeza mapato na thamani kwa walengwa wanaoshiriki katika Mradi. |
| **Vipengele:** 1) Miradi ya Jamii na 2) Vikundi; Uwezeshaji katika Ngazi ya Shehia, Wilaya na Kitaifa. |
| **Gharama kwa mwaka 2007/2008:** Tshs. 1,579,006,000 – Benki ya Dunia Tshs. 1,500,000 na SMZ Tshs. 79,006,000 |
| **Utekelezaji 2007/2008:** 1) Jumla Tshs 1,085.3 milioni zimepelekwa kutekeleza miradi ya jamii na vikundi vya wakulima sawa na asilimia 86.2 ya lengo. 2) Jumla ya Tshs.176.2 milioni sawa na asilimia 87.4 zimepelekwa Wilayani kwa kutekeleza kazi mbali mbali zilizopangwa. 3) laptop moja, computer 4, moving camera 1, photocopier 1 zimenunuliwa kwa matumizi ya afisi. 4) Taarifa zinaendelea kukusanywa na takwim za awali zinaonyesha mafanikio mazuri. 5) Mradi umetoa mafunzo ya Kilimo, Biashara na Masoko kwa wanajamii katika shehia 65 Unguja na Pemba. 6) Ziara za mafunzo zimefanyika kwa wakulima wa unguja na Pemba kutembeleana.<br>Aidha, Maafisa 12 kutoka Zanzibar wamefanya ziara ya kutembelea miradi ya PADEP Wilayani Uyui na Urambo – Mkoani Tabora. |
| **Gharama kwa mwaka 2008/2009:** Tshs. 1,220,973,610 – Benki ya Dunia Tshs. 1.180,973,610 na SMZ 40,000,000 |
| **Malengo kwa mwaka 2008/2009:**<br>1) Kufanya tathmini ya shughuli na matokeo yaliopatikana kuanzia mwaka 2003/08. 2) Kushajiisha dhana ya Mradi kwenye Wilaya nne mpya zilizochaguliwa kutekeleza PADEP. 3) Kuwafunza DMT na DFT filosofia ya Mradi pamoja na mbinu za PRA. 4) Kuzingatia uwezo wa wilaya nne mpya. 5) Kushajiisha wanajamii kwenye shehia mpya juu ya ujio wa PADEP. 6) Kufanya zoezi la PRA na Mafunzo ya Uandishi wa Miradi kwenye Shehia 32 Mpya. 7) Kupitisha na kuwapatia fedha wanajamii kwa ajili ya kutekeleza miradi yao. 8 Kufuatilia na kutathmini miradi mipya itakayoanzishwa. |

**KIAMBATISHO Na. 7. MRADI WA MPANGO MKUU WA UMWAGILIAJI MAJI**

| | |
|---|---|
| JINA LA MRADI | MRADI WA MPANGO MKUU WA UMWAGILAJI MAJI |
| MUDA WA MRADI | **2005-2020** |
| JUMLA YA GHARAMA | **Dola za kimarekani milioni 30** |
| WACHANGIAJI | **Serikali, wahisani na nguvu za wananchi** |

**LENGO KUU**

Kuimarisha kilimo cha u/maji nchini kwa kuongeza uzalishaji,pato la wakulima wadogo wadogo na uhakika wa chakula.

**MALENGO MAALUM**

- Kuimarisha miundo mbinu ya U/Maji eneo lipatalo hekta 8,521
- Kuimarisha jumuiya za Wakulima wa U/Maji
- Kuelimisha wakulima kwa kutumia vishamba vya maonyesho.
- Kuwapatia wakulima nyenzo muhumu za kurahisisha Kilimo cha U/maji

**MAENEO YA MRADI**

Mradi utatekelezwa katika mabonde 57 Unguja na Pemba. Unazihusisha jumla ya 8521ha.

**VIPENGELE VYA MRADI**

- Kuwawezesha wakulima kulima mara mbili kwa mwaka
- Kuongeza uzalishaji wa mpunga, mboga mboga na mazao mengine kwa eneo dogo.
- Kuimarisha miundombinu ya U/Maji

**UTEKELEZAJI 2007/2008**

- **-**Wakulima3600 wlelimishwa na kuhamasishwa ishirini kati ya hao walipatiwa mafunzo T/bara.
- Misingi mikuu ya saruji ya U/Maji 1440m imejengwa.
- Ukarabati wa vigingi 24 vimejengwa.
- Transformer moja katika bonde la Kibokwa imewekwa
- Banda la pampu limejengwa na pampu imenunuliwa
- Ofisi moja mabwanashamba Pemba imeanza kujengwa.

**GHARAMA KWA MWAKA 2008- 2009 ni Tshs 55,000,000/=**

**MALENGO KWA MWAKA 2008-2009**

- Kuelimisha na kuhamasisha wakulima 4000 katika kilimo cha U/Maji
- Kuendeleza mashamba madogo madogo ya U/Maji
- Kuendeleza kilimo cha uvunaji wa maji ya mvua.(Rain water harvesting)
- Kuhamasisha umwagiliaji wa kutumia matone (Drip Irrigation)
- Kuwapatia mafunzo ya ndani na nje ya nchi wataalam wa Idara ya U/Maji
- Ukarabati majengo ya vituo vya U/Maji Cheju , Bumbwisudi,Mwera na Tibirinzi

**KIAMBATISHO Na. 8: MRADI WA MPANGO WA KILIMO CHA KISASA NA MAENDELEO YA KILIMO CHA UMWAGILAJI MAJI TANZANIA.**

| **MRADI WA MPANGO WA KILIMO CHA KISASA NA MAENDELEO YA KILIMO CHA UMWAGILAJI MAJI TANZANIA**. | |
|---|---|
| MUDA WA MRADI | 2007-2010 |
| JUMLA YA GHARAMA | Tshs 1,550,000,000/= |
| WACHANGIAJI - Serikali , Jamhuri ya Korea na nguvu za Wananchi | |
| **LENGO KUU**<br>Kuimarisha miundombinu ya kilimo cha u/maji katika bonde la Kibokwa na Bumbwisudi. | |
| **MALENGO MAALUM**<br>• Ujenzi wa misingi ya saruji 8000m<br>• Ukarabati wa misingi midogo ya U/Maji 650m na kutolea maji 560m<br>• Ujenzi wa barabara za shambani 350m<br>• Uwekaji wa pampu 11,transformer tatu za umeme<br>• Ujenzi wa vibanda vya pampu na ukarabati wa ghala<br>• Ujenzi wa Afisi ndogo Makao makuu Mbweni. | |
| **MAENEO YA MRADI** | Bumbwisudi 250ha na Kibokwa 52ha |
| GHARAMA KWA MWAKA 2007/2008<br>SMZ- Tshs 50,000,000/= KOICA- Tshs 195,000,000/= | |
| **UTEKELEZAJI 2007/2008**<br>Uchambuzi ya kinifu wa Mradi (Detail design study)<br>Ujenzi wa Afisi ndogo Makao Makuu Mbweni umeanza | |
| GHARAMA KWA MWAKA 2008- 2009 | SMZ -Tshs 68,000,000/= KOICA -Tshs 900,000,000/= |
| **MALENGO KWA MWAKA 2008-2009**<br>• Ujenzi wa misingi ya saruji 2900m<br>• Ujenzi wa misingi ya udongo 5340<br>• Ujenzi wa barabara za shambani 350m<br>• Ujenzi wa vigingi 130<br>• Ukarabati wa misingi kutolea maji 600m<br>• Uchimbaji wa visima sita ( Kibokwa -2 na B/sudi – 4 )<br>• Ukarabati wa visima 8<br>• Uwekaji wa pampu 11<br>• Uwekaji wa transformer nne za umeme (mbili mpya na<br>• mbili kongwe)<br>• Ujenzi wa vibanda vya pampu 8<br>• - Kuendeleza Ujenzi wa Afisi ndogo Makao makuu Mbweni. | |

**KIAMBATISHO Na. 9. MRADI WA UHIFADHI WA MISITU NA MAENDELEO YA JAMII**

| | |
|---|---|
| **Jina la Mradi** | **MRADI WA UHIFADHI WA MISITU NA MAENDELEO YA JAMII** |
| Muda wa mradi | Wa kuendelea |
| Wachangiaji | SMZ |
| Lengo kuu | Kurejesha hali ya kijani ya mji wa Zanzibar |
| Malengo maalum | Kusimamia, kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za misitu kwa faida za kijamii, kiuchumi na kimazingira kwa manufaa ya Taifa. |
| Maeneo ya kazi | Wilaya zote za Unguja |
| Gharama kwa mwaka 2007/08 | Tshs. 86,100,000/- kutoka SMZ |

Utekelezaji 2007/08

- Kuotesha miche 647,700 ya misitu, matunda na viungo sawa na asilimia 65 ya lengo
- Ekari 200 zimepandwa miti katika mashamba ya misitu ya serikali
- Ekari 83 za miti iliyokomaa ilivunwa.
- Barabara ya kukinga moto kilomita 12 za mraba zimelimwa.
- Ekari 240 za miti zililimwa majalbe, ekari 240 zilifyekewa na ekari 15 za miche jamii ya michungwa, miembe na viungo zimepaliliwa.
- Hadi kufikia April 08 jumla ya shilingi 45,738,184/- sawa na asilimia 53 ya lengo zimepatikana

**Gharama kwa mwaka 2008/09** Tshs 128.,000,000.

**Malengo ya mwaka 2008/09**

- Kuotesha miche 1,000,000 ya misitu, matunda, viungo na mapambo katika vitalu vya Serikali.
- Kupanda miche ya misitu ekari 200, kuvuna miti iliyokomaa ekari 120 na kutayarisha barabara za kukinga moto kilomita 40 za mraba.
- Kulima majalbe ekari 400 na kufyekea miti ekari 200 pamoja na kuhudumia mashamba ya Masingini na Bungi.

**KIAMBATISHO Na. 10: MRADI WA MPANGO WA TAIFA WA UIMARISHAJI MIKARAFUU**

| | |
|---|---|
| **Jina la Mradi** | **MRADI WA MPANGO WA TAIFA WA UIMARISHAJI MIKARAFUU** |
| Muda wa mradi | Wa kuendelea |
| Wachangiaji | SMZ na Shirika la ZSTC |
| Lengo kuu | Kuongeza pato la wananchi kwa lengo la kupunguza umaskini |
| **Malengo maalum**<br>1. Kufufua na kuendeleza mashamba ya mikarafuu kwa kupanda miche mipya katika maeneo yaliowazi.<br>2. Kufanya utafiti wa zao hilo na mazao mengine ya Biashara hasa viungo ambavyo vinaweza kuota katika mashamba ya mikarafuu. | |
| **Maeneo ya kazi** | Wilaya zote za Unguja na Pemba |
| **Vipengele vya Mradi**<br>1. Kuotesha miche ya mikarafuu kwa wingi ili kutosheleza mahitaji ya wakulima<br>2. Kutoa elimu ya kilimo mchanganyiko cha karafuu na mazao ya viungo | |
| **Gharama kwa mwaka 2007/08 -** | Tshs. 92,440,000 |
| **Utekelezaji 2007/08**<br>▪ Miche 200,000 ya mikarafuu imeoteshwa sawa na asilimia 67 ya lengo<br>▪ Mafunzo ya utunzaji na utayarishaji bora wa mazao ya viungo kabla na baada ya mavuno yametolewa kwa wakulima 20 wa Wilaya ya Kati na 30 kwa Mkoa wa Kaskazini, Unguja na 35 kwa Mkoa wa Kusini na 25 kwa Kaskazini, Pemba<br>▪ Hadi kufikia April 08 jumla ya shilingi 3,000,000 zimepatikana kutoka Serikalini sawa na asilimia 3.2 ya lengo | |
| **Gharama kwa mwaka 2008/09** - | Tshs. 40,000,000 |
| **Malengo ya mwaka 2008/09**<br>▪ Kuzalisha miche 3000,000 ya mikarafuu.<br>▪ Kutoa mafunzo ya kilimo mchanganyiko cha mikarafuu na mazao mengine ya viungo.<br>▪ Kuanza matayarisho ya kuesabu mikarafuu (Inventory)<br>▪ Kutoa mafunzo ya uchumaji na ukaushaji wa zao la karafuu. | |

## KIAMBATISHO Na. 11: MRADI WA USIMAMIZI WA MAZINGIRA YA BAHARI NA UKANDA WA PWANI (MACEMP)

<table>
<tr><td>Jina la Mradi</td><td>MRADI WA USIMAMIZI WA MAZINGIRA YA BAHARI NA UKANDA WA PWANI (MACEMP)</td></tr>
<tr><td>Muda wa Mradi</td><td>Miaka 6 (2005-2011)</td></tr>
<tr><td colspan="2">Jumla ya Gharama<br>JShillingi bilioni 31.34 - Benki ya Dunia bilioni 25.194 ; GEF : bilioni 5.187 na JSDF: milioni 959</td></tr>
<tr><td colspan="2">Wachangiaji - Benki ya Dunia, Shirika la Mazingira Duniani “GEF” na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii wa Japan ‘JSDF’</td></tr>
<tr><td>Lengo kuu</td><td>Kupunguza umaskini kwa wananchi waishio katika ukanda wa pwani na Taifa kwa jumla ; na kuhifadhi mazingira ya bahari na ukanda wa pwani.</td></tr>
<tr><td colspan="2">Malengo Maalum<br>1. Kuhifadhi mazingira ya bahari na ukanda wa pwani<br>2. Usimamizi bora wa ukanda wa uchumi wa Bahari kuu.<br>3. Kujenga uwezo wa wanajamii katika matumizi bora ya maliasili kwa lengo la kupunguza uharibifu wa mazingira na maliasili na hatimae kupunguza umaskini.<br>4. Kuimarisha huduma za miundombinu na kuimarisha uwezo wa taasisi na jamii.</td></tr>
<tr><td colspan="2">Maeneo ya Mradi<br>Wilaya 10 za Unguja na Pemba na maeneo ya bahari yaliyomo katika udhibiti wa Tanzania.</td></tr>
<tr><td colspan="2">Vipengele vya Mradi<br>1. Usimamizi wa ukanda wa uchumi wa Bahari Kuu (EEZ).<br>2. Usimamizi wa eneo la bahari na ukanda wa pwani.<br>3. Mfuko wa Vijiji vya Ukanda wa Pwani.<br>4. Uratibu wa mradi.</td></tr>
<tr><td colspan="2">Gharama kwa Mwaka 2007/2008<br>Shillingi: 6,209,553,700 IDA: Shillingi 4,485,176,800, GEF: Shillingi 866,665,800 JSDF: Shillingi 824,781,100 na SMZ: Shillingi 32,930,000.00</td></tr>
<tr><td colspan="2">Utekelezaji 2007/2008<br>1. Jumla ya miradi ya jamii 73 (48 Pemba na 25 Unguja) yenye thamani ya Shs. 1,348,535,535/- imepatiwa fedha na mradi wa MACEMP kupitia TASAF.<br>2. Ujumbe wa watendaji wa Zanzibar ulitembelea nchini China kujifunza kuhusu mwenendo wa biashara ya mwani.<br>3. Utafiti wa mahitaji ya kimafunzo, Elimu asilia, na taarifa za awali kwa ajili ya kutathmini mradi umefanyika. Hatua za kulifanya eneo la hifadhi ya mkondo wa Pemba (PECCA) kuwa eneo la urithi wa dunia zinaendelea kwa mashirikiano na taasisi nyengine husika.<br>4. Tangazo la kazi ya kutayarisha michoro ya jengo la afisi ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA) limetangazwa na utaratibu wa manunuzi wa kumpata mtaalam wa michoro ya ujenzi unaendelea.<br>5. Watendaji wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira walihudhuria mafunzo ya usimamizi wa maeneo ya ukanda wa pwani, mafunzo ya kufanya tathmini ya miradi “project monitoring and evaluation”, mafunzo ya secretarieti. Aidha, Ujumbe wa watendaji wa Zanzibar ulitembelea nchini China kujifunza kuhusu mwenendo wa biashara ya mwani.</td></tr>
</table>

**Malengo ya Mwaka 2008/2009**

1. Kuendelea na taratibu za manunuzi (procurement) ya kumpata mjenzi wa majengo ya Afisi za Idara ya Uvuvi (Unguja na Pemba) pamoja na Afisi za maeneo ya hifadhi za bahari za Menai, PECCA, na Mnemba-Ghuba ya Chwaka.
2. Kuendelea na taratibu za kumpata mchoraji na mjenzi wa Jengo la Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari kuu Tanzania litakalojengwa Zanzibar.
3. Kuwezesha taratibu za ujenzi wa soko na maabara ya samaki.
4. Kusaidia jamii ya ukanda wa pwani kwa kuwapatia miradi midogo midogo kupitia TASAF. Kiasi cha miradi 90 inatarajiwa kutekelezwa ambayo inahusiana na sekta ya uvuvi, utalii, mambo ya kale na misitu.
5. Kuipatia jamii ya ukanda wa pwani katika maeneo ya hifadhi za baharini ya Menai, PECCA, na Mnemba-Ghuba ya Chwaka miradi midogo midogo kupitia mfuko wa Maendeleo wa Japani (JSDF). Kiasi cha miradi 30 inatarajiwa kutekelezwa.
6. Kuwezesha watendaji wa taasisi zinazotekeleza mradi wa MACEMP kupata mafunzo ndani na nje ya nchi.
7. Kuiwezesha Idara ya Mazingira kuandaa mpango wa usimamizi wa ukanda wa pwani (ICM action plan).
8. Kuendelea na taratibu za kumpata mtaalamu wa kutayarisha mpango mkuu wa usimamizi (General Management Plan "GMP") wa maeneo ya hifadhi za bahari za Menai, Mnemba-Ghuba ya Chwaka na PECCA.
9. Kuwezesha kufanyika utafiti wa kijamii na bioanuai katika maeneo mawili yanayopendekezwa kuwa hifadhi za baharini ambayo ni bahari ya visiwa vya mji mkongwe na Tumbatu.
10. Kuanza hatua za awali za kuanzisha mfuko maalum "Marine Legacy Fund" utakaoendeleza shughuli usimamizi wa mazingira ya bahari na ukanda wa pwani.
11. Kufanyakazi na sekta binafsi ili kuongeza ushiriki na mchango wa wadau mbali mbali katika maendeleo ya jamii "Public Private sector Partnership".
12. Kuziwezesha taasisi zinazotekeleza mradi kutekeleza majukumu yao.

## KIAMBATISHO Na. 12. TAARIFA YA MAPATO

| KASMA | CHANZO CHA MAPATO | MAKADIRIO YA MWAKA 2007/08 | FEDHA ZILIZOKUSANYWA KUANZIA JULAI 2007,HADI APRIL 08 | Sawa na Asilimia | MAKADIRIO YA MWAKA 2008/09 |
|---|---|---|---|---|---|
| 37044 | MAPATO MENGINEYO | 321,200,000 | 139,968,537 | 44 | 285,200,000 |
| 37012 | UKAGUZI MAZAO | 13,500,000 | 5,349,500 | 40 | 16,600,000 |
| 37015 | MAUZAJI YA MAZAO NA MICHE | 9,500,000 | 5,475,100 | 58 | 10,600,000 |
| 37018 | MAUZAJI YA MBOLEA | 12,000,000 | - | - | 12,000,000 |
| * | ADA YA UINGIZAJI WATALII | | | | 10,000,000 |
| 37020 | UTIBABU WA VINYAMA | 35,000,000 | 44,003,230 | 126 | 35,000,000 |
| 28001 | MAZAO YA MISITU | 132,000,000 | 89,707,682 | 68 | 132,000,000 |
| 28002 | ADA UUZAJI MAWE/KOKOTO MCHANGA | 82,500,000 | 61,132,255 | 74 | - |
| 37062 | MAUZAJI YA MICHE | 15,130,000 | 7,757,600 | 51 | 15,130,000 |
| 32006 | LESENI YA UVUVI | 14,000,000 | 12,762,750 | 91 | 14,400,000 |
| 32007 | MAZAO YA BAHARINI | 56,000,000 | 23,778,030 | 42 | 56,000,000 |
| 37095 | ADA YA HIFADHI YA MAZINGIRA | 700,000 | 6,007,000 | 858 | 6,447,000 |
| 37096 | ADA YA UKAGUZI WA MAZINGIRA | 1,500,000 | 2,055,000 | 137 | 2,625,000 |
| * | VIBALI VYA USAFIRISHAJI WA MALI ZISIZOREJESHEKA | - | | | 97,000,000 |
| 35015 | ADA YA UANDIKISHAJI VYAMA VYA USHIRIKA | 1,700,000 | 1,738,000 | 102 | 1,700,000 |
| 35016 | ADA YA UKAGUZI WA VYAMA VYA USHIRIKA | 1,350,000 | 109,000 | 8 | 2,000,000 |
| | **JUMLA** | **696,080,000** | **399,843,684** | **57** | **696,702,000** |

KIAMBATISHO Na. 13: TAARIFA ZA KAZI ZA MAENDELEO (MIRADI)

| TAARIFA ZA KAZI ZA MAENDELEO (MIRADI) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| KASMA | JINA LA MRADI | MAKADIRIO YA MWAKA 2007/2008 | FEDHA ZILIZOTOLEWA KUANZIA JULAI 2007 HADI APRIL, 2008 | % | MAPENDEKEZO YA MWAKA 2008/2009 |
| 61205 | Programu ya Mifugo(ASDP-L) | 94,064,000.00 | 69,000,000.00 | 73 | 55,000,000.00 |
| 61225 | Programu ya Kilimo (ASSP) | 279,304,000.00 | 138,000,000.00 | 49 | 125,000,000.00 |
| 61300 | Programu ya Kilimo (HIV/AIDS) | 19,730,000.00 | 17,385,388.25 | 88 | 15,000,000.00 |
| 61310 | Mradi wa uhakika wa chakula na lishe | - | - | | 74,000,000.00 |
| 61320 | Mradi Usarifu wa mazao ya Kilimo | - | - | | 35,000,000.00 |
| 61330 | Mradi wa Miundo Mbinu ya kilimo. | - | - | | 25,000,000.00 |
| 61260 | Mradi wa Ushirikishwaji wa ( PADEP) | 79,006,000.00 | 40,286,299.00 | 51 | 40,000,000.00 |
| 61206 | Mradi wa Kudhibiti kichaa cha mbwa | 12,000,000.00 | 12,000,000.00 | 100 | 10,000,000.00 |
| 61207 | Upandishaji Ngo'mbe kwa Sindano | 132,912,000.00 | 7,300,000.00 | 5 | 508,000,000.00 |
| 61240 | Mradi wa Kuimarisha Mikarafuu | 92,440,000.00 | 13,000,000.00 | 14 | 40,000,000.00 |
| 61250 | Program ya Uwiano na Usimamizi wa Maliasili | 86,109,000.00 | 73,347,552.10 | 76 | 128,000,000.00 |
| 61270 | Mradi wa Ghuba ya Minai | 34,000,000.00 | 23,448,890.20 | 68 | 20,000,000.00 |
| 61290 | Mradi wa (MACEMP) | 32,930,000.00 | 24,196,000.00 | 73 | 10,000,000.00 |
| 61215 | Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Kilimo cha U/Maji | 84,818,000.00 | 78,637,533.70 | 92 | 147,000,000.00 |
| 61216 | Mradi wa Kilimo cha Kisasa na Uendelezaji wa Kilimo cha U/Maji | 50,000,000.00 | 50,000,000.00 | 100 | 68,000,000.00 |
| | **JUMLA** | **997,313,000.00** | **546,601,663.25** | **54** | **1,300,000,000.00** |